SportPesa
TZS. 482,274,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**IMF** yaipatia Tanzania mkopo wa trilioni 1.3/- kukabili athari corona

UKURASA 3



**Enrique amuita Guardiola kuinoa Hispania**

UKURASA 20

Nipashe
Alhamisi Septemba 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580698
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mapingamizi serikali tozo miamala yatupwa

• **Korti** Kuu yasema hayana msingi, LHRC sasa kuwasilisha hoja kupinga... *Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akivalishwa mavazi ya kimila kuwa Chifu Mkuu wa Machifu wote Tanzania na kuitwa jina la Hangaya lenye maana ya nyota inayong`aa, wakati wa Tamasha la Utamaduni kwenye Viwanja vya Redcross Kisesa Magu, mkoani Mwanza jana. **PICHA: IKULU**.

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**
**ACT YAMTAKA WAZIRI KIKAO MSAJILI, POLISI**
CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema kuwa katika kikao cha Msajili...

**UKURASA WA 4**
**MATAPELI WAIBUKA MRADI MAGOMENI KOTA**
WATU wanaojitambulisha kama maofisa wa Wakala wa Majengo...

## Samia mkuu wa machifu Tanzania

UKURASA 3



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (katikati), akitembelea maonyesho ya bidhaa mbalimbali, zilizotengenezwa na wajasiriamali wanawake, baada ya kuzindua Kongamano la Wanawake na Biashara, jijini Dodoma jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapata neema ya kuwezeshwa kiuchumi

UKURASA 2

**MICHEZO** **GOMES APAGAWA UBORA NYOTA SIMBA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ACT-Wazalendo yamtaka waziri kikao na msajili

**Na Donald Lukele,** TUDARCo

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimesema kuwa katika kikao cha Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jeshi la Polisi na Vyama vya Siasa, ni muhimu akawapo Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene.

Aidha, kimesema kama anataka kuwepo kwa suluhisho la mgogoro baina ya Polisi na Vyama vya Siasa kuhusu mikutano ya kisiasa ni lazima pande hizo ziwapo kwa kuwa polisi ni watekelezaji wa maagizo kutoka juu.

Akizungumza na Nipashe, Katibu Mwenezi wa ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, alisema katika kufikisha ujumbe huo tayari, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, amemwandikia msajili kumtaka waziri huyo awepo kwenye kikao hicho.

Kauli ya chama hicho, imekuja siku chache baada ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mtungi, kusema ataitisha kikao maalum cha wadau wa siasa kutafuta suluhu ya mivutano iliyojitokeza baina ya polisi na vyama vya siasa, hususan vyama vinapotaka kufanya makongamano au mikutano ya ndani.

"Jana (Juzi) Mwenyekiti Kabwe amemwandikia msajili kumtaka kuhakikisha waziri anakuwapo kwenye kikao hicho sababu polisi ni chombo kinachopokea amri tu kuzuia mikutano kutoka kwa viongozi hususan wakuu wa mikoa na wilaya, uwapo wake utasaidia kukumbushana ukweli maeneo ambayo sheria na kanuni mbalimbali hazifatwi na vipi zitekelezwe," alisema Shaibu.

Aliongeza kuwa hatua hiyo ina lenga kuleta mwanga juu ya hatima ya uhuru wa kikatiba juu ya makongamano na mikutano ya kisiasa nchini, kwa kuwa suala hili limepigiwa kelele hususan vyama vya upinzani kwa takribani miaka sita sasa.

Kwa mujibu wa Shaibu, ni mapema sana kuweka matumaini makubwa juu ya kikao hicho lakini chama chake kitashiriki na kupeleka mapendezo pamoja na kufikisha hoja husika, ili kuleta msukumo wa mageuzi ya uendeshaji wa siasa nchini kwani kukimbia meza ya mazungumzo siyo suluhisho.

Juzi, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alisema kauli ya Msajili kuhusu mikutano na makongamano inakiuka sheria na kanuni.

Aidha, siku hiyo hiyo Msajili Jaji Mutungi, alitoa taarifa kwa umma na kueleza chama hicho kimepotosha kauli yake kwa kuwa hajazuia mikutano wala makongamano, bali amevishauri vyama kwa kipindi vinapojaribu kupata ufumbuzi wa mvutano uliopo ni busara vyama kujizuia kufanyua shughuli zitakazosababisha kurudi kwenye hali hiyo.

# Mapingamizi ya serikali tozo yatupwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu imetupilia mbali mapingamizi matatu ya serikali katika kesi ya kupinga tozo za miamala ya simu iliyofunguliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa sababu hayana sifa za kuwa pingamizi.

Uamuzi huo mdogo ulitolewa na Jaji John Mgeta ambaye ameyatupilia mbali maombi yaliyofunguliwa na Charles Odero, akipinga tozo kwa sababu kiapo kina kasoro. Jaji Mgeta aliwaalika mawakili katika maombi ya LHRC kuwasilisha hoja za kuomba ruhusa ya kupinga tozo hizo.

Mapingamizi yaliyotupwa yaliwasilishwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, akionyesha shauri hilo halina msingi lifutwe.

Alidai maombi hayana msingi kwa sababu hakuna uamuzi wowote uliotolewa na walalamikiwa ambao unahitaji kufutwa na mahakama, walichofanya walalamikiwa ni kutimiza wajibu wao kikatiba kutafuta chanzo cha mapato.

Sababu ya pili alidai maombi hayana msingi kwa sababu yaliwasilishwa na taasisi bila kuwa na maamuzi ya bodi, wakati kisheria taasisi inapotaka kufungua shauri ni lazima kuwapo na maamuzi ya kutoka kwenye bodi.

Wakili Malata alidai mlalamikaji hajaonyesha namna gani anavyoathirika na hakuonyesha anaathirika vipi na wala hakuonesha maslahi yake.

Akijibu, Wakili Mpale Mpoki alidai sheria inaruhusu ikiwamo ile iliyoanzisha tozo kupingwa mahakamani.

Alidai, hoja kuhusu uamuzi wa bodi siyo pingamizi la kisheria kwa sababu ni suala linalohitaji ushahidi na kwamba aliyeapa katika kiapo kaonyesha dalili kwa namna gani kaathirika na alifanya hivyo kwa niaba ya umma na ana maslahi katika shauri hilo.

Mahakama katika uamuzi wake ilikubaliana na hoja za waombaji na kutupilia mbali mapingamizi ya serikali kwa kukosa sifa.

Katika shauri hilo LHRC inaomba ruhusa ya mahakama ili wawasilishe maombi ya mapitio kuhusu Sheria ya Mfumo wa Taifa wa Malipo pamoja na kanuni zake zilizoweka tozo katika miamala ya fedha kwa njia ya simu.

Shauri hilo lilitokana na kupitishwa kwa mapendekezo ya bajeti ya serikali ya mwaka 2020/2021 na Sheria ya Fedha iliyosababisha kuweka tozo ambayo anaitaja kuwa mzigo kwa wananchi wa kawaida na wafanyabiashara ndogondogo.

Maombi yatasikilizwa Septemba 20, mwaka huu, shauri lilifunguliwa dhidi ya Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Katika hatua nyingine Mahakama Kuu ilitupilia mbali shauri la kupinga tozo ya miamala lililofungiliwa na Charles Odero kwa sababu hati ya kiapo ina kasoro.

Jaji John Mgeta baada ya kupitia mapingamizi matatu ya Jamhuri ambao walitaka maombi hayo yatupwe na hoja zilizowasilishwa ilikubaliana na pingamizi la pili kwamba hati ya kiapo ina kasoro na kutupa mapingamizi mawili.

Alisema baadhi ya aya zenye kasoro ziondolewa na kwamba aya zilizobakia haziwezi kusapoti maombi. "Aya zenye kasoro zikiondolewa kiapo kinabakia hakina kitu, kwa kuondolewa kwa aya hizo, maombi yaliyopo mahakamani hayana sifa yanakosa miguu ya kusimamia," alisema Jaji Mgeta.

Kutokana na upungufu huo mahakama ilitupilia mbali maombi hayo bila gharama.

Wakili Malata alidai katika mapingamizi kwamba kanuni zipo kwa mujibu wa sheria, uamuzi umelenga kuiwezesha serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati kwa wananchi.

Alidai kanuni zilikuwa shirikishi kwa kuwa zilishirikisha wawakilishi wa wananchi.

Upande wa serikali uliendelea kudai kanuni husika zina mamlaka kisheria na kikatiba katika uanzishwaji na pia madai hayako sawa mbele ya mahakama kwa kuwa yana upungufu mwingi kisheria ikiwa ni pamoja na mlalamikaji kushindwa kuonyesha kwa namna gani ameathirika na kanuni.

Serikali inadai malalamiko yaliyopo mahakamani yanahusu uvunjwaji wa Katiba na sheria ambayo yanaweza kusikilizwa na Mahakama Kuu ikikaa kama Mahakama ya Kikatiba na si Mahakama Kuu ya kawaida.



Mwenyekiti wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe (kulia), akiambatana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TCD, Lawrance Mallawa, wakiwa kwenye mazungumzo na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, baada ya TCD kumtembelea katika ofisi ndogo za makao makuu ya CCM, Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapata neema ya kuwezeshwa kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAWAKE nchini wamepata fursa mbalimbali za kuwezeshwa kiuchumi, baada ya Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kutangaza mkakati madhubuti wa kuwa taasisi kinara ya kuwahudumia.

Imeelezwa kuwa mkakati huo utasaidia kulikwamua kundi hilo kiuchumi kupitia suluhisho la kifedha kwao kwa kuzingatia changamoto zao kama wajasiriamali.

Katika kutimiza azma hiyo, benki hiyo jana ilizindua Kongamano la Wanawake na Biashara jijini Dodoma, ambalo litakuwa jukwaa maalum la kuchochea maendeleo yao binafsi, familia, jamii na taifa kwa ujumla.

Maofisa waandamizi wa benki hiyo walisema ili lengo hilo kuwa na matokeo chanya, midahalo kama hiyo itafanyika pia Zanzibar, Morogoro, Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam.

Katika makongamano hayo, wanawake hasa wajasiriamali watapata fursa ya kuifahamu vizuri TCB na huduma zake wezeshi, huku wakibadilishana mawazo na uzoefu wa mambo mbalimbali.

Walisema lengo la jukwaa hilo si tu kuwawezesha wanawake wa kitanzania kiuchumi, bali pia kuwaimarisha kifedha na kuwajenga kibiashara ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

Mgeni rasmi kwenye kongamano hilo la ufunguzi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ambaye aliipongeza Benki ya TCB na viongozi wake kwa kuanzisha utaratibu huo wa kimaendeleo na kiuwezeshaji.

Mtaka alisema ubunifu huo wa hali ya juu ni nyenzo mahususi ya kuwakomboa wanawake kifedha na kuwafanya kuwa nguvu kubwa ya kiuchumi itakayokuwa chachu muhimu ya maendeleo nchini.

Mtaka aliongeza kuwa Jukwaa la Wanawake na Biashara la TCB linaendana na mpango wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuongeza ushiriki wa wanawake katika kusimamia na kumiliki uchumi wa taifa. Jukwaa hilo jipya litaendeleza huduma jumuishi kwa ajili ya wanawake kupitia mikakati mbalimbali itakayowawezesha kufungua uwezo wao wa ujasiriamali na kuchangia mabadiliko kuanzia ngazi ya kaya hadi taifa.

Pia litajikita zaidi kwenye ufumbuzi wa changamoto zinazozikabili biashara zinazomilikiwa na kuongozwa na kinamama.

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi, benki hiyo inawajibika kuupa kipaumbele uwezeshaji wa wanawake na maendeleo yao baada ya serikali kuziunganisha shughuli zake na za iliyokuwa Benki ya Wanawake Tanzania (TWB).

Moshingi alibainisha kuwa mali na amana za TCB ni Sh. Trilioni 1.04 na Sh. bilioni 888 mtawalia kufikia mwishoni mwa mwaka jana wakati faida kabla ya kodi ya TCB iliongezeka kutoka Sh. milioni 400 mwaka 2007 hadi Sh. bilioni 21 mwaka 2020, na kwamba ukopeshaji ndani ya kipindi hicho ulikuwa hadi Sh. bilioni 618 Sh. bilioni 36.

HABARI KITAIFA

# Samia asimikwa kiongozi wa machifu

**Na Waandishi Wetu**

UMOJA wa Machifu Tanzania (UMT), umemsimika Rais Samia Suluhu Hassan kuwa kiongozi wa machifu nchini huku ukimpa jina maalumu 'Hangaya' lenye maana ya nyota ya asubuhi inayong'ara.

Hafla hiyo ilifanyika jana katika viwanja vya Red Cross Bujora, wilayani Kisesa mkoani Mwanza na kuhudhuriwa na viongozi wa kimila, kidini, serikali na wananchi.

Rais Samia alisimikwa rasmi jana na kiongozi wa Machifu wa Wasukuma, Charles Dotto Itare na tukio hilo lilishuhudiwa na viongozi mbalimbali wa kimila na serikali. Akizungumza baada ya kumsimika uongozi wa kimila, Itare, alisema, kuanzia sasa Rais Samia amekuwa kiongozi wao.

Alimvisha Rais Samia vazi jekundu kama ishara ya ulinzi wa nchi, ngozi ya chui kama ishara upole, lakini mkali wakati anapolinda watoto wake na yai la mbuni ambalo linaashiria ulinzi wa watoto.

Akizungumza kabla ya kusimikwa kuwa kiongozi wa kimila, Rais Samia alisema utamaduni unasaidia kuleta amani pamoja na kudumisha mila na desturi kwa jamii ya kitanzania.

Aliwataka viongozi wa kimila kuendelea kusimamia maadili ya Mtanzania pamoja na kusuluhisha migogoro mbalimbali katika jamii.

Kadhalika, kwa kuwa matamasha hayo yana faida kwa jamii, aliagiza yafanyike nchi nzima ili kuendeleza na kudumisha mila na desturi.

Katika kuyapa heshima matamasha hayo, Rais Samia aliahidi kuandaa kikombe maalumu ili awe anashindanisha matamasha hayo na kumpata mshindi wa kila mwaka.

Alitoa mfano nchi kama ya Ethiopia ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikidumisha utamaduni wake na kwamba hivyo ni moja ya vivutio vya kitalii kwa nchi husika.

Aliwaomba Machifu hao kuendelea kuhamasisha jamii ili ijilinde na kuwakinga watu wengine dhidi ya ugonjwa wa corona.

Akizungumza baada ya kusimikwa rasmi kuwa kiongozi wa Machifu hapa nchini, Rais Samia ambaye kwa jina la kimila ni Hangaya, aliwashuruku viongozi hao kwa kumpa heshima hiyo.

"Nilipewa mamlaka kwa mujibu wa Katiba yetu, lakini leo mmenipa mamlaka haya ya kimila na kitamaduni, nawashukuruni sana," alisema.

Aliahidi kushirikiana na viongozi hao wa kimila ili kuhakikisha nchi inaenzi mambo ya mila na utamaduni wake.

Akizungumza katika tamasha hilo, Katibu wa UMT, Aron Mikomanga aliomba kupatiwa eneo la kujenga ofisi ya jijini Dodoma ili waweze kujipanua na kufanya shughuli zingine za kiuchumi.

Alimuomba Rais Samia kuwarudishia nyumba zao za Machifu zilizochukuliwa na serikali bila kuwalipa fidia katika maeneo mbalimbali.

Mkomanga aliomba Machifu kumiliki na kutumia nyara za serikali ikiwamo ngozi ya chui ili kukamilisha kazi zao wanazofanya katika jamii.

**●Habari hii imeandaliwa na Richard Makore na Rose Jacob, MWANZA**

# IMF yaipatia Tanzania mkopo wa tril. 1.3/- kukabili athari corona

**Na Romana Mallya**

BODI ya Wakurugenzi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), limeridhia mkopo nafuu kwa Tanzania wa Dola za Marekani milioni 567.25 (Sh. trilioni 1.3) kwa ajili ya kukabiliana na athari za corona.

Kutokana na mkopo huo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameziasa sekta zote zitakazopata fedha hizo kuzitumia kulingana na mpango ulioandaliwa kwa pamoja na sekta husika katika suala hilo.

Alisema fedha hizo zinapaswa kutumika kwa kuzingatia makubaliano ya serikali na IMF kama ilivyoainishwa kwenye barua ya dhamira ya serikali (Letter of Intent - LOI) ikiwa ni pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, fedha hizo zinajumuisha mkopo nafuu usio na riba kupitia dirisha la Rapid Credit Facility (RCF) wa Dola za Marekani milioni 189.08.

Pia alisema fedha hizo zinajumuisha mkopo nafuu wenye riba ndogo kupitia dirisha la Rapid Financing Instrument (RFI) wa dola za Marekani milioni 378.17.

"Fedha hizi zitatumika ndani ya mwaka huu wa fedha katika kukabiliana na athari za kiuchumi na kijamii zitokanazo na UVIKO-19," alisema.

Alisema sekta zitakazonufaika kulingana na makubaliano ya serikali na IMF ni afya, elimu, utalii, maji na kusaidia kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuwezesha makundi maalum ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

"Kila sekta itatumia fedha hizi kwenye masuala yanayolenga kukabiliana na na athari za corona ambapo pamoja na mambo mengine, sekta ya afya itanunua dawa na vifaa tiba vya kupambana na corona na kugharamia utekelezaji wa mpango wa chanjo," alisema.

Alisema sekta ya elimu itaweka mazingira yatakayowezesha wanafunzi kujifunza bila msongamano na kuchukua tahadhari ya maambukizi ya UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maboma ya shule na kuongeza madawati.

Mwaipaja alisema sekta ya maji itaongeza miundombinu ya maji itakayowezesha upatikanaji wa huduma ya maji tiririka kwa wingi zaidi mijini na vijijini; na mpango unaoendelea wa TASAF utaongezewa fedha ili kusaidia kaya maskini zilizoathirika na ugonjwa huo.

Aidha, alisema serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itawezeshwa pia kukabiliana na athari za corona katika sekta zilizoathirika ikiwa ni pamoja na afya, utalii na kilimo.

Taarifa ya IMF ilisema kuwa imeidhinisha fedha hizo ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kukabiliana na janga hilo kwa kushughulikia gharama za haraka za kiafya, kibinadamu na za kiuchumi.



# Matapeli waibuka mradi Magomeni Kota

**Na Maulid Mmbaga**

WATU wanaojitambulisha kama maofisa wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wamedaiwa kuwajazisha fomu na kuchukua fedha kutoka kwa wananchi kwa madai kuwa wanawapangisha nyumba katika mradi wa Magomeni Kota.

Kutokana na kuibuka kwa kundi hilo la watu, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewaonya na kusema watakaobainika watachukuliwa hatua za kisheria huku akiagiza vyombo vya usalama kuwasaka.

Akizungumza jana alipofika kukagua kota hizo, Makalla alisema majengo hayo yalitengenezwa, kwa ajili ya kaya 644 zinazotambulika kisheria, hivyo wananchi wawe makini wasikubali kutapeliwa kwa kuwa makazi hayo hayapangishwi kwa watu wasiokuwamo kwenye orodha ya kaya tajwa.

Makala alisema kutokana na uvumi na utapeli unaoendelea wa watu wanaoutumia mradi huo na kutangazia umma, kwamba wao wanafanya kazi TBA au wao ni mawakala wa kuwatafutia watu vyumba katika mradi huo, kimsingi eneo hilo hakuna vyumba vingine vya kupangishwa.

"Wananchi msidanganywe. Wale wote wanaochukua hela na kuwajazisha watu fomu ni matapeli na nielekeze vyombo vya ulinzi na usalama hasa Jeshi la Polisi na taasisi zingine zote kuwasaka hao matapeli wanaowaibia wananchi hela wakijifanya wanapangisha Magomeni Kota.

"Wananchi msikubali kuibiwa hela zenu na tutawakamata matapeli wote. Taarifa za awali zipo kwa hiyo natoa angalizo mtu usije ukapoteza hela yako. Nimeshapita vyumba vyote nimeviona hakuna sehemu ya kupangisha zaidi ya wakazi wanaotambulika," alisema Makalla.

Aliwataka wananchi wa Magomeni Kota wasubiri mradi huo utakapokamilika wataitwa, ili kukabidhiwa makazi yao na wataelezwa namna ya kuishi eneo hilo.

"Niwatoe hofu wakazi wa Magomeni Kota, ambao ni kaya 644 waliopisha mradi huu ufanyike kwamba wao wana haki ya kuwa miongoni mwa watakaofaidika na mradi huu, utakapokamilika watapewa utaratibu, hivyo muwe na subira," alisema Makalla.

Pia alitoa wito kwa TBA kutumia eneo lililopo kimkakati kwa kuwa sehemu iliyobaki ni kubwa na wanaweza wakafanya mambo mengine makubwa zaidi kutokana na Dar es Salaam kuwa na uhaba wa ardhi.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa TBA, Saidi Mndewe, alisema majengo hayo yamekamilika kwa asilimia 99 na kazi iliyobaki ni uunganishaji wa umeme, ambao mwisho wa mwezi huu utakuwa umekamilika na baada ya hapo wakazi wote watapewa semina ya kuwaelekeza kujua makazi yao na namna ya kuishi eneo hilo.

"Serikali imetumia gharama kubwa kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika, kwa hiyo ni jukumu kubwa kwa watakaokuwa wakazi kuhakikisha wanayatunza majengo haya na sisi tutaendelea kutupia jicho eneo hili, kuhakikisha huduma zote zinaenda vyema na majengo yanaendelea kudumu," alisema Mndewe.



Mkuu wa Mauzo wa Kanda ya Dar es Salaam na Pwani wa Vodacom Tanzania, Brigita Stephen (wapili kulia), akifafanua jambo kwa mkazi wa Bunju, kuhusu baadhi ya huduma zitolewazo na kampuni hiyo kwenye kampeni ya 'Kimbiza na 4G ya Ukweli', mkoani Dare es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Daktari aliyemfumua nyuzi mgonjwa awekwa kitimoto

**Na Mary Geofrey**

BARAZA la Madaktari Tanganyika (MCT), limemtaka daktari Kituo cha Afya Kerege, Korogwe mkoani Tanga, Jackson Meli, aliyefumua nyuzi kwenye jeraha la mgonjwa, kujieleza ndani ya siku 14.

MCT imemwandikia Meli notisi ya uchunguzi wa awali ya kuwasilisha kwa maandishi utetezi wake katika uda huo kwa mujibu wa Kanuni ya 7 (1) (b) ya Kanuni za Uendeshaji wa Mashauri ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi.

Taarifa iliyotolewa jana na Msajili wa Baraza hilo, Dk. David Mnzava, ilisema kitendo hicho ni cha uvunjifu wa maadili ya kitaaluma.

"Baada ya kupokea taarifa hii rasmi, baraza linaendelea na hatua za kimaadili kuhusu shauri tajwa na hatua kali kwa mujibu wa Sheria ya Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi Sura Na. 152 ya mwaka 2017, zitachukuliwa baada ya mtuhumiwa kukutwa na hatia," alisema Dk. Mnzava.

Alisema shauri tajwa limethibitishwa na mamlaka ya usimamizi ya mkoa, ambayo ni Ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa kwa barua yenye kumbukumbu namba RM/D.10/24 ya Septemba 6, mwaka huu.

Pia aliwataka wanataaluma wote kuzingatia Kanuni za Maadili ya utendaji wa Kitaaluma wa Udaktari, Udaktari wa Meno na Afya Shirikishi za mwaka 2005, katika maeneo yote yanayoongoza maadili ya kitaaluma.

Alisema ndani ya kanuni hizo kifungu cha 11.5.1 kinawaelekeza wanataaluma kuchukua hatua za haraka kwa wagonjwa wa dharura, bila kuchelewa na bila kuwa na ubaguzi wowote.

Aidha, aliwahimiza wanataaluma na wakuu wa vituo vya kutolea huduma za afya kuwasilisha taarifa za wagonjwa wasio na uwezo wa kuchangia huduma za afya kwa maofisa ustawi wa jamii katika vituo na maeneo husika, kwa ajili ya kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu huduma za msamaha.

Septemba 6, mwaka huu, Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kimelaani tukio hilo na kusema ni kinyume cha maadili ya taaluma.

Septemba 4, mwaka huu, kupitia mitandao ya kijamii, ilisambaa video iliyokuwa ikimuonyesha daktari huyo akifumua kidonda cha mgonjwa baada ya kukosa fedha za malipo.

## Watano wafa ajali Kenta, Fuso

**NaTumaini Mafie,** ARUSHA

WATU watano wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa katika ajali ya barabarani iliyohusisha Fuso na Kenta.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema ajali hiyo ilitokea jana alfajiri katika Barabara ya Arusha-Moshi eneo la Konoike kijiji cha Kolila, Tarafa ya King'ori, wilaya ya Arumeru.

Kamanda Masejo alisema ajali hiyo ilitokea baada ya magari mawili kugongana uso kwa uso ambapo gari lenye namba za usajili T.111 CUU aina ya Mitsubish Fuso lililokuwa linaendeshwa na Heriel Lyimo, mkazi wa Holili mkoani Kilimanjaro liligongana uso kwa uso na gari lenye namba za usajili T.612 BNN aina ya Mitsubish Canter iliyokuwa ikiendeshwa na Peter Mmasi.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa Fuso iliyokuwa inatokea Moshi kuelekea Arusha ambayo ilihama upande wa pili wa barabara na kugongana na Canter lililokuwa linatokea Arusha kuelekea Moshi.

Aidha baada ya magari hayo kugongana Fuso lilipitiliza na kuanguka kwenye mtaro uliopo pembezoni mwa barabara.

Waliokufa ni Peter Mmasi, Victor Kileo, Vivian Urio, na Isaack Temba ambao walikuwa abiria wa Canter na ni wakazi wa Baraa jijini Arusha,

Katika Fuso aliyefariki ni utingo wa gari hiyo aliyefahamika kwa jina moja la Idd, mkazi wa Himo mkoani Kilimanjaro.

Majeruhi ni Heriel Lyimo ambaye alipelekwa katika Hospitali ya KCMC mkoani Kilimanjaro kwa matibabu zaidi na miili imehifadhiwa katika hospitali ya Rufani ya Mount Meru jijini Arusha.

**HABARI KITAIFA**

## Ujerumani yaipa Tanzania bil. 67/- kukuza uhifadhi

**Na Christina Mwakangale**

UJERUMANI kupitia Benki ya Maendeleo Ujerumani (KfW), imeipatia Tanzania Sh. bilioni 67.82 kwa ajili ya mradi  wa kuendeleza uhifadhi endelevu wa maliasili, mifumo ya ikolojia na kulinda ushoroba wa wanyamapori Hifadhi za Taifa Serengeti na Katavi.

Katibu MKuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, ndiye aliyetia saini makubaliano hayo kwa niaba ya serikali wakati upande wa KfW iliwakilishwa na Mkurugenzi wa Afrika Mashariki na Umoja wa Afrika, Christoph Tiskens.

Tutuba alisema  msaada huo umekuja wakati mwafaka ili kuiinua sekta ya utalii iliyoathirika na Covid-19.

Tutuba alibainisha kwamba utekelezaji wa mradi huo utakuwa katika sehemu mbili na kwamba utaanza kwa kuendeleza na kuhifadhi maliasili Hifadhi ya Taifa ya Serengeti utakaogharimu Sh. bilioni 21.7 ukifuatiwa na mradi wa mifumo ya ikolojia Katavi hususani ushoroba wa Mahale.

Alisema lengo la mpago huo ni kuimarisha uhifadhi na kuwa madhubuti na usimamizi endelevu pamoja na kuchangia maendeleo ya kiuchumi hasa kwa wakazi wa wilaya tatu, zikiwamo Bariadi, Bunda, Serengeti na maeneo yote ya hifadhi.

"Mradi utahusisha ufadhili wa shughuli za kuongeza kipato katika wilaya husika na kuanzisha benki za kijamii za uhifadhi, uendeshaji, ujenzi wa miundombinu ukihussha madaraja, nyumba za hifadhi, matumizi bora ya maji na kusimamia utekelezaji sheria za hifadhi na ununuzi wa magari ya doria.

"Hatua hizo za mradi zitahusisha usimamizi wa maliasili, kuboresha maisha na matumizi bora ya ardhi na utoaji wa hatimiliki za kimila, kuongeza kipato. Lengo madhubuti ni usimamizi wa hifadhi za Taifa Katavi na Mhale, ushoroba wa wanyamapori na jamii zinazozunguka," alisema Tutuba.

Pia, alisema  ushirikiano wa Tanzania na Ujerumani uliodumu takribani miongo sita, umekuza na kuongeza miradi iliyofikia Sh. bilioni 678.54 katika kuendeleza sekta za maji, afya, nishati pamoja, usimamizi wa fedha za umma na matumizi endelevu ya maliasili.

Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alisema kuwekeana saini ili kutekeleza mradi huo kumefikiwa siku chache baada ya Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan, mapema mwezi huu.

# Daktari bingwa aanika chanzo cha watu kujiua

**Na Richard Makore,** MWANZA

TATIZO la watu kujiua limeelezwa kusababishwa na afya ya akili ikiwamo kuwa na wasiwasi, utumiaji wa dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia.

Daktari bingwa wa magonjwa ya afya ya akili kutoka Hospitali ya Rufani ya Bugando, Dk. Gema Peter, aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe, jijini hapo, kuhusu Siku ya Kupinga Watu Kujiua Duniani ambayo huadhimishwa Septemba 10, kila mwaka.

Alisema kila baada ya sekunde 40 mtu mmoja anajiua duniani kutokana na ugonjwa wa afya ya akili na hapa nchini watu wanane kati ya 100,000 wanajiua kwa mwaka kwa matatizo hayo.

Kadhalika, takwimu za mwaka 2019 zinaonyesha watu 700,000 hadi 1,000,000 wanajiua kila mwaka duniani kutokana na matatizo ya afya ya akili.

Dk. Gema alisema watu wengi wanajiua kutokana na matatizo ya afya ya akili na Shirika la Afya Duniani (WHO) na washirika wake kwa kutambua tatizo hilo walikubaliana kuadhimisha siku ya kupinga watu kujiua duniani.

Alisema vifo vitokanavyo na kujiua ni vingi, lakini kwa bahati mbaya jamii haipati taarifa kuhusu tatizo hilo.

Dk.  Gema alisema licha ya vifo kutokea kutokana na matatizo ya akili, lakini jamii bado imeendelea kuwaona watu wanaojiua kama ni wakosaji na kuamua kuwanyanyapaa.

Mtalaam huyo alisema mtu anayejiua huwa amekosa matumaini katika maisha yake na kumekuwa na visababishi vingi mpaka mtu kufikia kujiua.

Alitaja visababishi hivyo kuwa ni pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya, ulevi wa pombe wa kupindukia na mtu kupatwa magonjwa ya wasiwasi pamoja na magonjwa ya tabia.

Alifafanua kuwa ugonjwa wa wasiwasi ni mbaya na husababisha mtu kujiua kirahisi kwa kuwa muda wote anahisi ama kuona watu wabaya wanamsogelea kutaka kumuua na huamua kujiua kabla ya kufikiwa.

Kwa upande mwingine, Dk. Gema aliitaka jamii kuacha kuwapeleka wagonjwa hao kwa waganga wa kienyeji badala yake wawafikishe hospitalini kwa wakati ili wapate matibabu.

Alisema kwa sasa kuna watalaam wa kutosha katika kuhudumia wagonjwa wa afya ya akili na kwamba kinachotakiwa ni wananchi kuwahi kupata matibabu sahihi.




Mtendaji Mkuu wa Mahakama aliyemaliza muda wake, Mathias Kabunduguru (kulia), akimkabidhi vitendea kazi na ofisi, Mtendaji Mkuu mpya wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, katika hafla iliyofanyika Mahakama ya Rufani jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bosi mpya Mahakama ahimiza maadili

**Na Hellen Mwango**

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel, amewataka watumishi kutunza maadili ya utendaji na kamwe wasiruhusu uchafu ndani ya mahakama.

Kadhalika alisema ameagizwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kusimamia maslahi, wajibu wa watumishi wa mahakama nchini pamoja kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika mhimili huo.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akikabidhiwa ofisi na aliyekuwa Mtendaji Mkuu, Mathias Kabunduguru, baada ya kustaafu utumishi wa umma.

"Sitaruhusu uchafu kufanyika ndani ya mahakama badala yake nitasimamia iendelee kuwa safi kwa kusimamia maslahi, wajibu wa watumishi na matumizi ya TEHAMA," alisema.

Akifafanua alisema majukumu yake mengine ni, kusimamia haki ya kweli kwa mahakama iendelee kutolewa kwa wananchi na mazingira ya kufanya kazi kwa watumishi kuwa rafiki.

Alisema kwa sasa mahakama ina watumishi 5,835 kati ya idadi ya 10,350 wanaohitajika.

Mahakama za Mwanzo (960), Wilaya (119), Mkazi (Mkoa 29), Mahakama Kuu (17) na Mahakama ya Rufani (1).

Mapema Septemba Mosi, mwaka huu mahakama nchini imeanza rasmi kutumia mfumo wa Ofisi Mtandao ikiwa ni mafanikio ya matumizi ya TEHAMA.

Kwa upande wake Mtendaji Mkuu mstaafu, Kabunduguru alisema amewaasa watumishi wote kuisaidia serikali kutekeleza majukumu ili wananchi wote wapate huduma stahiki na kwa wakati sahihi.

Alisema katika miaka 34 ya utumishi wake wa umma amejifunza mengi na kwamba uadilifu ni msingi mkubwa wa utumishi na kufanikisha kutekeleza majumu kwa jamii.

Msajili Mkuu wa Mahakama Tanzania, Wilbard Chuma, alisema majukumu yao ya msingi ni kutoa haki kwa jamii.

"Utulivu na amani mnayoiona vinaimarishwa na mahakama zetu nchini kwa kuwa tunatimiza majukumu yetu kwa maadili ya kiwango cha juu," alisema Chuma.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# La biashara ya watoto lifuatiliwe kwa karibu

**JUZI** Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, lilieleza kuwakamata watu wawili kwa tuhuma za kuwatorosha watoto 11 wenye umri wa miaka 10 na 14, kwenye maeneo mbalimbali na kuwasafirisha kwenda kuwauza kwa wafugaji ili wakatumikie kuchunga mifuko.

Watuhumiwa hao walikamatwa Septemba 5, mwaka huu na kubainika kuwa baadhi ya watoto walitoroshwa kutoka kwa wazazi wao na wengine wale wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wanauza watoto hao kwa wafugaji walioko wilayani Mbarali kwa gharama kati ya Sh. 25,000 hadi 30,000, na kwamba kabla ya kuwauza waliwatumikisha kwenye shughuli za uzalishaji wakati wakiendelea kutafuta wateja wa kuwauzia. Aidha, baadhi ya watoto walisema walichukuliwa kwa kushawishiwa na wengine walichukuliwa kwa nguvu na kusafirishwa kwa kutumia pikipiki kwenda maeneo, ambayo watuhumiwa walikuwa wanawahifadhi.

Hili ni tukio moja kati ya mengi ambayo hujitokeza kwa watoto kupotea na kwenda kutumikishwa kwenye maeneo mbalimbali, ikiwamo shughuli za nyumbani, kutumikishwa kingono ambazo ni kinyume cha sheria ya mtoto.

Tukio hili linatoa picha halisi ya uwajibikaji wa wazazi katika kulinda na kutunza watoto wao kwa kuhakikisha wapata mahitaji ya msingi, ikiwamo elimu na siyo kutumikishwa kwenye migodi, nyumbani, sehemu za starehe na kwingine ambako hawastahili kuwapo. Unapotazama luninga ya ITV kila siku jioni utaona idadi ya wazazi ndugu na jamaa wanaotangaza kupotelewa kwa watu mbalimbali, hasa watoto ambao wengine huwapata, lakini wengine hawaonekani kabisa.

Tukio hili na mengine yanakumbusha wajibu wa wazazi kutunza watoto wao kufuatilia kwa karibu mienendo yao, ikiwamo maendeleo ya kitaaluma kama wanafika shuleni au la.

Kuna tatizo kubwa la baadhi ya wazazi kuzaa watoto na kukwepa jukumu la malezi kwa wengi kujilea wenyewe au kukosa msingi wa malezi kiasi kwamba ni rahisi kuchukuliwa na yeyote kama ilivyotokea wa watoto 11 walioibiwa na kwenda kuuzwa.

Kwa sasa matukio ya utapeli na kuiba watoto yanaongezeka kwa kuwa wanaofanya hivyo wanatengeneza mazingira ya kujipatia fedha huku watoto wakiumia kisaikolojia na kiafya.

Hii ni biashara haramu ya kusafirisha binadamu ambayo kimsingi hairuhusiwi kwa mujibu wa sheria za nchi, lakini inatuma salamu kuwa kuna tatizo kubwa hasa malezi na hali ngumu ya uchumi kwa baadhi ya wananchi.

Kwa mtazamo wetu ni muhimu kila mmoja akatimiza wajibu wake kwa ambaye ni mzazi au mlezi kumleta mwanaye ipasavyo, ikiwamo kufuatilia kwa karibu maisha yake kuliko kuacha kujilea, ili kuwa na vijana sahihi kwa taifa la kesho.


Watoto hao walitakiwa kuwa shuleni na siyo kwenda kutumikishwa, lakini ni muhimu vyombo vya dola vikafanya uchunguzi wa kina kwenye maeneo mengine kama ya mgodi ambalo kuna watoto wengi wanatumikishwa kwa ujira mdogo badala ya kwenda shuleni. Kwa mjini ikiwamo Dar es Salaam watoto wanatumika kuongoza ombaomba au kutumwa na wazazi wao kuomba au wanaosha vioo vya magari katika maeneo ya Makutano ya barabara za Mwenge na Salenda, na mbaya zaidi wengine ni watoto chini ya miaka nane.

Kwa mtazamo wetu ni muhimu sana jamii pia ikashiriki malezi ya watoto hao kwa kuwa wapo ambao wako kwenye mazingira magumu siyo kwa kupenda bali ni kwa sababu wazazi wamewatelekeza au wamefariki na kukosa mtu wa kuwatimizia mahitaji ya msingi kama ada na chakula.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukuaji wa teknolojia usigeuke halali ya uchafu mitandaoni

Na Ester Mgidula

**MIAKA** inapita sasa, suala la kuvuja picha na video za watu wakiwa faragha mtandaoni limeanza kutawala hata sura ya kuzoeleka sasa.

Miaka iliyopita, huenda hata kabla ya kizazi cha kwetu cha vijana wa leo hatujaanza kuwa na uelewa wa mengi, najua matukio mengi yalifanyika nyuma ya pazia na yalikemewa.

Ni kweli dunia imebadilika na kukua. Kuna maendeleo ya teknolojia nayo yamechangia kuongezeka matukio ninayodiriki kuyaita 'ya ajabu ajabu.'

Sisi vijana huku tuliko mtaani, tunaona namna wazazi wengi anavyopata tabu kuishi na kizazi kilichopo katika maelezo yao. Kwa ufupi, unaweza kukiita kizazi cha digitali.

Yapo mengi ya kushangaza yanayofanywa na Watanzania wanaoiga maisha ya walio ugenini, japo nakiri si wote wenye ninayoyaita 'ya ajabu ajabu.'

Niseme, kadri mambo hayo ya ajabu katika digitali yanavyopanuka, ndivyo hataninachodirikikukiita 'upuuzi' kwa wingi nao unawaingia akilini Watanzania.

Kama nilivyosema awali, kwamba maendeleo nayo huwa yana gharama zake. Mojawapo ndiyo hilo, matukio mengi ya faragha sasa yanakuwa kitu cha kawaida hadharani.

Nakumbuka wikiendi iliyopita kulikuwapo tamasha la soka la kimataifa likihusisha klabu ya nchini na wageni.

Baada ya tamasha hilo lililohusisha mchezo huo, kulisambaa video mitandaoni zikionyesha uchafu uliofanywa na moja ya mashabiki wa timu hizo jijini Dar es Salaam.

Hakika ni aibu, hata binafsi nikajikuta nakaa chini kutoa kauli rasmi ya masikitiko, wakati huohuo nikibaki pia sehemu ya jamii mitaani.

Kilichotokea, mada kuu inawaangukia watendaji wawili, jinsia ya kike na kiume ambao majina yao yanasambaa mtandaoni, zaidi nasikitika ni mwanama ambaye alistahili kuwa mstari wa mbele kutetea nafsi na faragha yake. Iko wazi inasikitisha sana.

Najiuliza, sijui tunaelekea wapi? Inawezekana kabisa, haya ndiyo malipo hasi ya maendeleo ya teknolojia. Naam, nikiri ndiyo! Lakini, bado kuna hitaji la serikali ijiongeze katika kuchukua kali dhidi ya matukio hayo ndani ya jamii zake.

Tusishangae, inaweza kutolewa hoja ya utetezi kwamba hayo ni mambo binafsi. Nami nakubali katika sura moja ya shilingi ni mambo binafsi, lakini katika sura pana imeshawasilishwa kwa maana na mtazamo wa maslahi ya umma.

Maudhui yaliyowasishwa yanasambaa kwa kasi kubwa, ndani ya dunia ambayo leo inasimama kama kijiji.

Siri ya madhara inazama mbali katika mtazamo, vijana wadogo ambao ni wanasimama katika kundi la wamiliki wa simu na uchafu huo unawafikia rasmi, kupitia ujumbe unaosambaa kwa kasi kubwa.

Maana yake sasa, nao ni mashuhuda na sio jabu hata wakawa washiriki katika ujumbe wa uchafu huo. Kuna uchafu mwingi unaosambazwa mitandaoni!

Najua ngazi tulioko leo, hatuwezi kurudi nyuma na kuishi ilivyokuwa miaka 20 au 30 kabla.

Ila tujiulize kila mmoja, kama wewe ndiyo mhusika umejirekodi uchafu aina hiyo, ukasambazwa na umati kushuhudia 'madudu' hayo, unajisikiaje?

Kuna watoto wanaokuhusu, kaka, dada zako, ndugu na jamaa wasiohesabika, kulingana na umaarufu na mtandao wako. Kwa ufupi inasikitisha na kuumiza sana.

Pamoja na uwapo wa mamlaka kama TCRA inayosimamia hayo, bado ninaamini kuna ya ziada kufanyika kudhibiti usambazaji wa ujumbe wa aina hiyo.

Kila jambo lina matokeo yake, hasi na chanya. Lakini, haiwezi kuwa hoja au kigezo cha jamii kuhalalisha uchafu kuwa sehemu ya maisha yetu.

Niseme, kuendekeza hayo ni namna ya kuiharibu jamii kwa kasi. Tujihadhari na kujiingiza shimoni.

## HABARI KITAIFA

# Sababu mfumuko bei kutobadilika zatajwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu imesema mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Agosti, 2021, umebaki kuwa asilimia 3.8.

Hali hiyo imetokana na kuongezeka na kupungua kwa baadhi ya bidhaa za vyakula na visivyokuwa vyakula, ikiwamo gharama za malazi kwenye nyumba za kulala wageni.

Bidhaa zingine zilizopunguza bei ni nafaka nyama, mboga na maharage huku mavazi, mkaa, gesi na malazi hayo vikitajwa kuongeza mfumuko huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu na Jamii, Ruth Minja, alisema mfumuko huo umebaki kuwa asilimia 3.8 kama ilivyokuwa kwa mwaka ulioishia Julai 2021.

Minja alisema hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Agosti 2021 imekuwa sawa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioshia Julai 2021.

"Mfumuko huo umechangiwa na uongezeko na kupungua kwa bei kwa baadhi ya bidhaa za vyakula kama mahindi, unga wa mahindi kwa asilimia 4.7 nyama asilimia 6.3, mboga asilimia 2.3 na maharagwe kwa asilimia 4.7."

"Kwa upande mwingine baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilioongezeka bei ni pamoja na mavazi, asilimia 4.7 mkaa asilimia 1.9 gesi asilimia 2.1 kodi ya pango asilimia 5.1 na gharama za malazi kwenye nyumba za kulala wageni asilimia 5.3,"alisema Minja.

Hata hivyo, alisema kwa bidhaa za vyakula na vinvywaji baridi kwa Agosti 2021, umepungua hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 5.1 kwa mwaka ulioishia Julai 2021,

Mkurugenzi huyo pia alisema hali ya mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka ulioishia Agosti 2021, nchini Kenya umeongezeka hadi kufikia asilimia 6.57 kutoka asilimia 6.55 kwa mwaka ulioishia Jualai 2021.

Kwa upande wa Uganda, mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2021 umepungua hadi asilimia 1.9 kutoka asilimia 2.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2021.

Naye Mkurugenzi wa Takwimu za Uchumi wa NBS, Daniel Msolwa, alisema licha ya kuwapo kwa ugonjwa wa corona hapa nchini, mwenendo wa viashiria vya kiuchumi vya muda mfupi Januari hadi Juni 2021 umeendelea kuimarika.

# PM ataka elimu kukomesha migogoro

**Rehema Mbinda na Patson Andugalile,** TUDARCo

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka wadau wa sekta ya mifugo nchini kuongeza jitihada katika kuelimisha na kuhamasisha ufugaji ili kuepuka migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Akifungua mkutano wa siku mbili wa wadau hao jana Dar es Salaam, alisema sekta ya mifuko ni muhimu na ya kipaumbele kwa serikali, kwa kuwa imewekwa mipango ya kuiwezesha kuchangia upasavyo kuwakwamua wananchi kiuchumi na kutoa malighafi kwenye viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo.

"Hakikisheni wafugaji wanaelimishwa na kuhamasishwa kufuga kulingana na maeneo waliyonayo. Halmashauri nazo zihamasishe ufugaji ambao hautachochea migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi,"alisema na kuongeza;

"Viongozi na watendaji wa serikali hakikisheni mnashirikiana kwa karibu na sekta binafsi wakiwamo wafugaji katika kuwawezesha kuwekeza na kuendeleza ujenzi wa miundombonu ya mifugo ikiwamo majosho, malambo, maeneo ya malisho na visima vya maji."

Aidha, alisema serikali imeweka juhudi katika sekta hiyo kwa kuwa inaamini ushiriki wa moja kwa moja wa serikali ni muhimu kupitia kuelekeza nguvu kwenye ufugaji wa kisasa, ili kufikia malengo yenye tija katika kukuza uchumi na kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja.

Waziri Mkuu aliziagiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinashirikiana na wadau wa sekta binafsi katika kuwawezesha na kuendeleza maeneo ya malisho pamoja na kuwahamasisha wafugaji kuboresha mifugo yao ili kuongeza tija katika uzalishaji. Pia, alitoa onyo jamii ya wafugaji kuacha tabia ya kuwapa watoto kazi za kuchunga badala yake wajikite kuhakikisha wanapata elimu bora kwa manufaa ya baadaye.

Awali, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema lengo la mkutano huo ni kutoa nafasi kwa wadau kufahamu fursa, mikakati na changamoto zilizopo na kujadili namna ya kuziondoa.

" Hii ni sekta muhimu lakini bado imekuwa na malengo na mafanikio madogo katika pato la taifa sasa upo umuhimu wa kukutana na kubadilishana mawazo ili kuongeza faida katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla,"alisema.

Naye, Mwenyekiti wa chama cha wafugaji Tanzania, Jeremiah Wambura, aliiomba serikali kuzitupia jicho baadhi ya taasisi zinazowabana wafugaji na kuwanyima stahiki zao, jambo linalokwamisha ukuaji wa sekta hiyo.

# Itifaki kutatua kero mazao kuzuiwa mipakani yaridhiwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limeridhia itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Viwango vya Afya ya Mimea, Wanyama na Usalama wa Chakula ambayo pamoja na mambo mengine, itaharakisha maendeleo katika Sekta ya Kilimo na kukua kwa biashara.

Waziri wa Kilimo, Profesa Adolf Mkenda, akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, maelezo kuhusu itifaki hiyo, alisema chimbuko la azimio la kuridhia itifaki hiyo ni Ibara ya 151 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inayobainisha kuwa nchi wanachama zitaandaa itifaki katika maeneo yote ya ushirikiano pale inapobidi.

Alitaja matokeo na faida ya kuridhia itifaki hiyo kuwa Tanzania itaimarisha na kuboresha afya na usafi wa mimea, wanyama na usalama wa chakula.

Profesa Mkenda alisema utekelezaji wa itifaki hiyo pia utaharakisha maendeleo katika Sekta ya Kilimo, ubora wa mazao, usalama wa chakula na kukua kwa biashara.

"Baadhi ya matokeo yatakayotokana na kuridhiwa kwa itifaki ni pamoja na kukua kwa biashara ya chakula na mazao ya kilimo miongoni mwa nchi wanachama wa jumuiya. "Kutaongezeka kwa fursa na bidhaa za Tanzania kuingia kwenye soko la jumuiya bila vikwazo ikiwa ni matokeo ya ulinganifu wa viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula.

"Itifaki itatoa fursa ya kuimarisha ushirikiano katika kujenga uwezo wa wataalamu na utafiti unaolenga viwango vya afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula," alifafanua.

Waziri huyo aliongeza kuwa itifaki hiyo itawezesha nchi kuwa na nguvu ya pamoja na nchi nyingine katika kutetea bidhaa zinazosafirishwa kutoka ndani ya jumuiya kuingia katika soko la kimataifa.

Pia kuimarisha uratibu kwa kuwa na mwongozo wa pamoja ndani ya jumuiya kuhusu afya ya mimea, wanyama na usalama wa chakula. Alisema faida nyingine ni kuwapo kwa fursa ya pamoja katika kanda ya kujilinda dhidi ya magonjwa na visumbufu vya mimea na wanyama.

Vilevile, kuboresha afya na usafi wa mimea wanyama na usalama wa chakula na hivyo kuimarisha kwa maisha ya wananchi.

"Itifaki itawezesha kupungua kwa vikwazo visivyo vya kiforodha mipakani vinavyohusu biashara ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kutokana na uwazi na tathmini ya athari kulingana na makubaliano yanayohusu masuala ya viwango vya afya ya mimea, wanyama na chakula.

"Kuoanisha taratibu za uthibiti na ukaguzi wa mazao mipakani zitakazoondoa matakwa yasiyo ya lazima yanayoambatana na milolongo mirefu ya taratibu pamoja na kuimarasha utengamano wa kikanda," alisema.

Waziri huyo alisema uwianishaji wa sera, sheria na kanuni kwa mujibu wa itifaki hiyo unazingatia maslahi ya nchi na jumuiya kwa ujumla ambapo tahadhari dhidi ya uingizaji wa mazao na bidhaa zilizobadilishwa vinasaba (GMO) zitaendelea kuchukuliwa kwa kuzingatia sheria na msimamo wa Tanzania.

"Tanzania itakuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba EAC haitumiki kama eneo la kuingiza bidhaa na mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi zinazoweza kuhatarisha usalama wa chakula, usalama wan chi, wanyama na mazingira," alisema.


NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA (NHC)

1. Kama mnavyofahamu kuanzia tarehe 20 Agosti, 2021, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianza kukusanya kodi ya majengo kwa kutumia njia ya ununuzi wa umeme (LUKU).
2. Tunapenda kuwafahamisha wapangaji wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwa Shirika limefanya mazungumzo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kukubaliana kuhusu namna bora ya kutoza kodi ya majengo kupitia LUKU.
3. Ili kuwezesha zoezi la kubaini na kupendekeza TANESCO mita zitakazotumika kukatwa kodi ya majengo, tunaomba kila mpangaji kuwasilisha namba ya mita anayotumia kulipia umeme kwenye mikoa ya Shirika la Nyumba la Taifa anakopanga ueleze jina linalosomeka kwenye Mita husika.
4. Ni muhimu kila mpangaji kuzingatia maelekezo haya ili kuepusha usumbufu kwa mpangaji na Shirika. Mita ambayo haitawasilishwa na mpangaji kwenye Mkoa husika ndani ya wiki mbili kuanzia tarehe ya tangazo hili au kupendekezwa na NHC kutumika kulipia kodi ya majengo, Shirika halitawajibika kumrejeshea mpangaji husika fedha zitakazoendelea kukatwa na TANESCO.
5. Tunapenda kuwafahamisha wapangaji wetu kuwa Shirika linaratibu makato yote yatakayofanywa na TANESCO kwa wapangaji na linaandaa utaratibu muafaka wa kufidia makato hayo kupitia kodi zao.
6. Tunawashukuru wapangaji wote kwa kuendelea kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa wakati na kuliwezesha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuwaletea Watanzania maendeleo kwenye sekta ya nyumba.

**IMETOLEWA NA:**
**OFISI YA HABARI NA UHUSIANO**
**SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA**

216449702

# ‘Wabunge wanawake wekeni itikadi pembeni’

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WABUNGE wanawake wametakiwa kuweka kando itikadi zao za kisiasa bungeni ili kusimamia hoja na sheria zinazohusu wanawake.

Mkuu wa Mkoa wa Singida mstaafu, Dk. Rehema Nchimbi, aliyasema hayo jijini hapa kwenye semina kwa wabunge wanawake iliyoandaliwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA).

Alisema wabunge na viongozi wengine wanawake wana jukumu la kushirikiana na katika kuhakikisha wanasimamia ajenda za wanawake kwenye kutunga sheria au upitishaji wa hoja.

“Wanawake tunaendelea kubaki kuwa wanawake. Tuhakikishe tunapokuwa kwenye maeneo ya kupitisha au kutunga sheria, tutangulize umoja wetu. Tukigawanyika kwa misingi ya kidini au kisiasa tunaoathirika ni wanawake wenyewe,” alisema.

Pia aliwataka wanawake kushirikiana katika uandaaji na utungaji sera, sheria, miradi na programu za maendeleo kwenye eneo hilo ili kuleta usawa wa kijinsia kwa manufaa ya wanawake viongozi wa kisiasa na kijamii wanayoiwakilisha.

Naye Mratibu wa Miradi wa TAWLA, Josephine Arnold, alisema semina hiyo inalengo la kuwaleta pamoja wabunge wanawake ili kuwaongezea uwezo kwenye masuala ya uongozi na umuhimu wa kutetea ajenda ya wanawake ndani ya Bunge.

Alisema TAWLA inatambua na kuthamini kazi na mchango wa wabunge hao katika kutetea haki za wanawake ndani na nje ya Bunge ambayo inategemewa kuleta maendeleo chanya kama itazingatia usawa wa kijinsia katika uandaaji wa sera, sheria, miradi na programu za maendeleo katika ngazi zote.

Alisema dira ya TAWLA ni kuhamasisha jamii, kulinda na kutetea haki za wanawake na dhamira kuu ni kutetea na kulinda haki za wanawake na utawala bora kupitia uwezo wa kisheria.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge Wanawake (TWPG), Sophia Mwakagenda, aliishukuru TAWLA kwa kuwajengea uwezo katika utendaji wao wa kazi.

Mwakagenda alikiomba chama hicho kuwa karibu na wabunge ili kuwasaidia katika kushauriana kuhusu miswada inayopelekwa bungeni kwa sababu wao wanaueleewa mkubwa wa kisheria katika kutetea wanawake.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Benki ya Mwanga Hakika (MHB), Project Massawe, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano mkuu wa kwanza wa wanahisa utakaofanyika Septemba 18, mwaka huu, wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro. Kushoto ni Katibu wa Benki hiyo, Marry Kissanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tamasha kukutanisha wavuvi 10,000 Zanzibar

**Na Beatrice Shayo,** ZANZIBAR

TAMASHA la kimataifa linalohusu rasilimali na vyakula baharini, linatarajia kuwakutanisha wavuvi 10,000 na kutoa ajira za muda zisizopungua 16,322 katika mkoa wa Kaskazini Unguja.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mkuu wa Mkoa huo, Ayoub Mohammed Mahmoud, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo linalojulikana kama ‘Zanzibar Sea Food Festival’ ambalo litafanyika kwa siku mbili kuanzia Oktoba 8, mwaka huu.

Alisema tamasha hilo limebuniwa kwa lengo la kuunga mkono juhudi za utekelezaji wa sera za serikali chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Ayoub alisema Zanzibar ni kisiwa kilichobarikiwa kuwa na rasilimali nyingi za bahari zenye kutoa fursa katika kuendeleza sera ya uchumi mpya unaojulikana kama uchumi wa buluu.

Serikali, alisema imeweka mkazo mkubwa katika kukuza uchumi na uwekezaji kupitia maliasili za bahari, ikiwamo kuendeleza sekta za utalii, uvuvi na mazao ya baharini, sanaa, burudani na utamaduni wa watu wa Pwani.

“Tamasha letu hili litahusisha makundi mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kwa kuwaweka pamoja katika eneo la ufukwe wa Kendwa kwa muda wa siku mbili mchana na usiku,”alisema Ayoub.

Aliyataja makundi yatakayoshiriki katika tamasha hilo ni wavuvi, watalii, wasanii, wawekezaji, watembeza wageni, taasisi za fedha, mashirika ya teknolojia ya habari, mawasiliano, kampuni za vinywaji mbalimbali, hoteli za kitalii na migahawa, wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania.

Pia alisema fursa mbalimbali zitapatikana katika tamasha hilo ambazo zitasaidia jamii hususani wakazi wa mkoa wa Kaskazini Unguja.

“Miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na mauzo ya samaki yasiyopungua tani 30, kuwakutanisha na kuwaunganisha kibiashara wavuvi wasiopungua 10,000 na wawekezaji wa hoteli za kitalii 127, ujenzi na ukarabati wa madarasa yasiyopungua 150, ajira za muda zisizopungua 16,322, ujenzi wa barabara ya lami ya kilometa 2.5, maonyesho ya kazi za wavuvi na wajasiriamali pamoja na kazi za uhifadhi wa mazingira,” alisema.

Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema una eneo kubwa la fukwe zenye ubora duniani na wigo mpana wa kufanya shughuli za uvuvi na viwanda vya uchakataji wa mazao ya bahari jambo ambalo litasababisha tamasha hilo kujenga uwezo wa uchumi mdogo miongoni mwa wananchi unaotokana na sekta ya bahari, sambamba na kuutangaza Mkoa wa Zanzibar duniani.

Aidha, alisema tamasha hilo linatarajia kuwakutanisha watu kutoka mataifa mbalimbali wasiopungua 30,000 kwa siku zote mbili.

Naye Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema katika tamasha hilo watatatoa elimu ya matumizi sahihi ya fedha.

# Kizimbani tuhuma za kutoroka nchini

**Na Beatrice Inyasi,** TUDARCo

WATU sita wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa tuhuma za kutaka kuondoka nchini kinyume cha sheria kwenda Afrika Kusini.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rita Tarimo, Wakili wa Serikali Shija Sitta alidai watuhumiwa hao walitenda kosa hilo Septemba 7, mwaka huu.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Yassin Abdallah (30), Ernest Said (23), John Ugo (30), Alex Ulunga (28), Ally Athumani (33) na Stration Rweyemamu ( 33), wote wakazi wa Dar es Salaam.

Wakili Sitta alidai Septemba 8, mwaka huu, watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, wakiondoka nchini bila kufuata utaratibu.

Aidha, watuhumiwa Abdallah, Said na Ugo walikiri kosa hilo na kutakiwa kulipa faini ya Sh. 300,000 kila mmoja au kwenda jela mwaka mmoja.

Aidha, watuhumiwa Ulunga, Athumani na Rweyemamu walikana kosa hilo na walirudishwa mahabusu.

Kesi hiyo imeahirishwa mpaka Septemba 22, mwaka huu itakapotajwa tena.

# Wajasiriamali wapata fedha ubora wa bidhaa

Na Mwandishi Wetu, MWANZA

SERIKALI imetenga fungu maalum kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo kuthibitisha ubora wa bidhaa zao kwa kupatiwa huduma hiyo bila gharama yoyote kwa miaka mitatu.

Hayo yalisemwa na Ofisa Masoko wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Deborah Haule, wakati akizungumza na washiriki na wananchi waliotembelea maonyesho ya Biashara ya Afrika Mashariki yaliyofanyika jijini Mwanza, na kwamba huduma ya uthibitishaji ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali wadogo ni bure isipokuwa kinachotakiwa ni wajasiriamali kupata barua ya utambulisho kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kuipeleka TBS ambako mchakato wa kuwapatia alama ya ubora unaanza mara moja.

Haule alisema TBS inatambua mchango wa wajasiriamali katika kukuza pato la taifa na kutengeneza ajira kwa wananchi wengi ndiyo maana kuna mchakato endelevu wa kutoa elimu kwa wajasiriamali kwa kuwa na hilo ni sehemu ya majukumu ya shirika ili kupata alama ya ubora.

Aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali wa mikoa ya Kanda ya Ziwa kujitokeza kwa wingi kupata huduma TBS kwa ajili ya kuthibitisha ubora wa bidhaa wanazozalisha.

Haule alisema TBS imeshiriki katika maonyesho hayo kwa lengo la kuwasogezea huduma karibu wajasiriamali na wafanyabiashara kwa ujumla na kutoa elimu ya viwango ili kuzalisha bidhaa bora na salama zinazoweza kushindana katika soko la kimataifa.

# Kilosa wataka bajeti kukarabati visima maji

Na Christina Haule, MOROGORO

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mkoani hapa, limetakiwa kutenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 kukarabati miradi ya visima vya maji (Magole ADP), ili iwe endelevu.

Akizungumza wakati Shirika la World Vision Tanzania likikabidhi mradi huo waliouhudumia tangu mwaka 1996 -2021 na kuwa jumla ya miaka 25 chini ya ufadhili wa Marekani, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga, alisema kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo kuwapo ni muhimu kuendelea kukarabatiwa, ili iwe endelevu.

Alisema ipo miradi ya visima vya maji inayoweza kufa kama isipokuwa na matengenezo ya wakati maalum na kupoteza maana ya kuwapo kwa miradi hiyo katika maeneo hayo.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la World Vision Tanzania, Gilbert Kamanga, aliiomba halmashauri ya wilaya hiyo kutenga bajeti, kwa ajili ya usimamizi wa miradi wanayoiacha, ambayo imegharimu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 11 (sawa Sh. trilioni 12).

Kamanga alisema fedha hizo zimetumika katika kuimarisha masuala ya maendeleo kwa jamii ikiwamo kuimarisha uelewa wananchi, miradi mbalimbali kiafya, kielimu, kilimo, ufugaji na utunzaji wa mazingira.

# Msajili ashauriwa mkutano wa vyama vya siasa, polisi

Na Sabato Kasika

MSAJILI wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi, ameshauriwa kuharakisha mkutano wake na Jeshi la Polisi na viongozi wa vyama vya siasa ili kumaliza utata unaosababisha kuzuiwa kwa mikutano ya vyama vya siasa.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipokuwa akizungumzia mkutano huo, ambao bado haujapangiwa tarehe.

"Anachotaka kufanya msajili ni jambo sahihi, lakini ni vyema angeharakisha kufanya hivyo, kwani kumekuwapo na utata kwenye mikutano ya kisiasa hasa pale polisi wanapoingilia kati na kuivunja," alisema Ngawaiya.

Mwenyekiti huyo alisema, mikutano ya vyama hivyo ipo kisheria na kwamba Sheria namba tano ya vyama hivyo ya mwaka 1992, inaruhusu huku ikielekeza vyama vya siasa kutoa taarifa polisi saa 48 kabla.

"Hapa vyama vyote vinahusika kikiwamo chama tawala, ambapo baada ya taarifa, polisi wanatakiwa kufika kwenye mkutano kutoa ulinzi ili likitokea jambo lolote ambalo ni hatari waweze kukabiliana nalo," alisema.

Alisema, kinyume chake, mikutano imekuwa ikizuiwa huku zikitajwa sababu mbalimbali, hali ambayo anafafanua kuwa imeleta mkanganyiko na sintofahamu, na kwamba ujio wa mkutano huo unaweza kuleta suluhu. "Ni vyema mkutano huo ukafanyika haraka, kwani ninaamini unaweza kuleta suluhu kwa kumaliza utata ambao umekuwa ukisababisha malumbano kati ya wanasiasa na vyombo vya dola," alisema.

Ngawaiya alisema, yeye ni miongoni mwa wanasiasa ambao wamekumbana kadhia ya kuzuiwa na polisi kufanya mikutano ya kisiasa wakati huo alipokuwa kwenye vyama vya NCCR- Mageuzi na hata TLP.

"Ushindani katika siasa ni jambo lisiloepukika, ndiyo msingi wa uwepo vyama vingi vinavyoshindana kwa sera, hoja, kupingana na kukosoana, sisi CEGODETA tunashauri mkanganyiko huo umalizwe haraka," alisema.

Juzi msajili wa vyama hivyo, alikaririwa na vyombo vya habari akisema kuwa anatarajia kukutanisha Jeshi la Polisi na viongozi wa vyama vya siasa ili kuweka vizuri utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa bila kukwaruzana.

Alisema, mkutano huo utajadili jinsi ya kuondoa kile kinachoonekana kuwa upo uhasama kati ya Jeshi la Polisi na vyama vya siasa na namna ya kuweka vizuri utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa.

Kwa mujibu wa msajili huyo, mvutano kati ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi, umeanza kujenga taswira hasi kwa umma, na kwamba asingependa kuona watu waogopa, kila mkutano wa siasa, polisi wamejaa, kila shughuli ya wanasiasa polisi wanajaa.

Hata hivyo, CHADEMA, imesema haishiriki kwenye mkutano ulioitishwa na msajili, kwa madai kwamba, kwa kipindi cha miaka sita, Jeshi la Polisi limefanya mambo yanayokiuka katiba na sheria bila kuonywa.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi Mambo ya Nje, John Mrema, ndiye aliyetoa kauli hiyo wakati akizungumza na wanahabari, jijini Dar es Salaam wakati akitoa msimamo wa chama hicho.



Mbunge wa Liwale mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka, akipata chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona jijini Dodoma juzi, huku akitoa wito kwa wakazi wa jimbo lake kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata ili kuchanjwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aporwa mil.9/- na wanaodaiwa majambazi

Na Thobias Mwanakatwe

WATU wanne wanaosadikiwa kuwa ni majambazi wakiwa na silaha za moto wamemvamia mfanyabiashara na kumpora kiasi cha Sh. 9,000,000.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, akizungumza na gazeti hili kwa simu jana, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 4 usiku, mjini Vwawa, wilayani Mbozi.

Alimtaja aliyeporwa kuwa ni mfanyabiashara wa miamala ya fedha, Elia Ndimbo, mkazi wa mtaa wa Ilolo, wilayani Mbozi.

Kamanda Magomi alisema mfanyabiashara huyo aliporwa fedha hizo wakati akirejea nyumbani kwake baada ya kufunga biashara yake.

Alisema baada ya watu hao kumvamia mfanyabiashara huyo karibu na nyumbani kwake, walifanikiwa kupora kiasi hicho cha fedha, simu nne za mkononi, pamoja na mashine za kutolea fedha na kutokomea kusikojulikana.

Alisema Jeshi la Polisi baada ya kupewa taarifa lilianza kufuatilia na kufanikiwa kupata simu na mashine za kutolea fedha zikiwa zimetelekezwa.

"Kuhusu taarifa za majambazi kurusha risasi ovyo, tumeambiwa kuwa kulisikia mlipuko, sasa bado tunaendelea na uchunguzi, ili kujua ilikuwa ni risasi au kitu gani," alisema.

Pia, Kamanda Magomi alisema hadi sasa hakuna mtu yeyote aliyekamatwa na jeshi hilo linaendelea na msako, ili kuhakikisha wahusika wote wa tukio hilo wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Hivi karibuni kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya watu kulalamika kuvunjiwa nyumba na maduka kisha kuibiwa katika miji ya Tunduma, Vwawa na Mlowo, mkoani hapa.

HABARI BUNGENI

# Maboresho Sheria ya Ndoa yaja

SERIKALI imeahidi kuwasilisha bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa baada ya kukamilisha michakato mbalimbali ikiwamo kushirikisha wadau wengi kutoa maoni yao.

Wizara ya Katiba na Sheria, iliyasema hayo bungeni jana katika majibu ya swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zainab Katimba.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka Muswada wa Sheria ya Ndoa Bungeni ili kurekebisha vifungu vinavyohusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri chini ya miaka 18.

Katika majibu ya wizara hiyo, ilisema Muswada wa Sheria ya Ndoa ulifikishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Mwezi Februari, 2021.

Ilifafanua kuwa ulifikishwa kwa kamati hiyo kufuatia maamuzi ya Mahakama ya Rufani katika kesi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi Rebecca Gyumi, Rufani namba 204/2017 na namba 5/2016 ya Mahakama Kuu iliyotaka Sheria ya Ndoa ifanyiwe marekebisho ili mtoto wa kike aolewe akiwa na miaka 18.

Ilisema kamati baada ya mapitio iliona upo uhitaji wa kushirikisha wadau wengi zaidi ili kupata maoni zaidi.

Hata hivyo, serikali inaendelea na zoezi la kushirikisha wadau ambapo hadi sasa serikali imeweza kufanya mkutano na viongozi wa dini katika Mkoa wa Dar es Salaam Machi 17, 2021.

Pia ilisema mkutano wa pili ulifanyika jijini Dodoma Julai 2, 2021, uliojumuisha wabunge wa mkoa wa Dodoma na viongozi wa Halmashauri ya Mkoa wa Dodoma.

Aidha, ilisema kurejeshwa kwa Muswada huo serikalini kulitokana na unyeti wa jambo lenyewe.

Iliiambia Bunge kuwa serikali itakapokamilisha michakato iliyoelekezwa na Kamati ya Bunge, Muswada huo utawasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria na kuwasilisha mbele ya Bunge kwa ajili ya kutunga sheria husika.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wiliam Lukuvi, akizungumza wakati alipokuwa akijibu maswali ya wabunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rais Samia afuta hati mashamba 11

RAIS Samia Suluhu Hassan amebatilisha umiliki wa mashamba 11 yenye ekari 24,159 mkoani Morogoro kutokana na wamiliki wake kukiuka masharti ya umiliki.

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ilitoa kauli hiyo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itafanya tathmini ya mashamba pori yasiyoendelezwa mkoani humo.

Kwa mujibu wa wizara hiyo, mashamba hayo yalibatilishwa Aprili, 2021.

Ilisema katika kipindi cha mwezi Julai 2020 hadi Juni 2021, jumla ya mashamba 160 yamekaguliwa katika mkoa huo.

Kati ya mashamba hayo, mashamba 123 yanapatikana Kilosa, Kilombero (3), Mvomero (13) na Morogoro (21).

Ilieleza kuwa serikali inafanya utaratibu wa kuyapanga na kuyapima kwa ajili ya matumizi ya wananchi, uwekezaji na ardhi ya akiba.

Hata hivyo, ilisema kwa sasa serikali inaendelea na ukaguzi wa mashamba mengine katika Wilaya za Morogoro (mashamba 44) na Mvomero (mashamba 86).

Baada ya ukaguzi huo hatua za kisheria zitafuata kwa wamiliki waliokiuka masharti ya umiliki na kusisitiza ukaguzi huo ni endelevu likiwa na maslahi mapana ya taifa ya kuhakikisha wanaondoa migogoro inayojitokeza kwa kuwapo mashamba yasiyoendelezwa ipasavyo.




## SIDO, WMA zaagizwa kasi vifungashio mafuta

WIZARA ya Viwanda na Biashara imeliagiza Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Wakala wa Vipimo (WMA) kuharakisha urekebishaji wa vifungashio vya mafuta ya mawese ili wakulima mkoani Kigoma wasiendelee kunyonywa.

Wizara hiyo ilibainisha hayo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), Assa Makanika.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali imefikia hatua gani katika kurekebisha vifungashio vya mafuta ya mawese kwa kuwa wananchi wanaumizwa na kunyonywa kupitia vifungashio vinavyotumika sasa.

Wizara hiyo iliitaka SIDO kuzalisha kwa wingi vifungashio hivyo na kuviuza kwa bei nafuu kwa wazalishaji wa mafuta hayo nchini ili kutekeleza kwa vitendo agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilolitoa kwenye ziara yake mkoani Kigoma mwezi Februari, 2021.

Awali, ilisema SIDO Mkoa wa Kigoma imetengeneza sampuli za vifungashio vya mafuta ya mawese vitakavyotumiwa na wakulima.

Ilisema kwa kuanzia SIDO imetengeneza sampuli za vifungashio vya lita tano na lita 20 na vipo kwenye mfumo wa ndoo ya chuma.

Hata hivyo, ilisema hatua inayofuata ni sampuli za vifungashio kuwasilishwa WMA kwa ajili ya uhakiki.

Aidha, baada ya WMA kuhakiki vifungashio hivyo, itawasilisha sampuli hizo za vifungashio kwa SIDO ili kuzalishwa kwa wingi.

## Ataka masomo ya maadili, afya

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga, ameitaka serikali kuanzisha somo maalum la maadili na afya kuanzia shule za msingi ili kukabiliana na mabadiliko ya maumbile ya hisia za mwili.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema masomo hayo yatasaidia mtoto anapoanza kukua ikiwa ni njia ya kukabiliana na tatizo la watoto kuanza kushiriki mapenzi mapema.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilisema inatambua umuhimu wa kufundisha maadili kwa mtoto ili kukabiliana na mabadiliko ya maumbile ya hisia za mwili kama njia ya kukabiliana na tatizo la watoto kuanza kushiriki mapenzi mapema.

Ilisema mitaala ya elimu inayotumika kwa sasa imetilia msisitizo kuhusu masuala ya maadili katika ngazi zote za elimu.

Ilibainisha kuwa katika ngazi ya elimu ya msingi kuna somo la uraia na maadili ambalo ni somo la lazima kwa wanafunzi wote kuanzia darasa la tatu.

Vile vile, ilisema suala la mabadiliko ya maumbile ya mtoto,hufundishwa katika somo la Sayansi na Teknolojia, Stadi za Kazi, na Uraia na Maadili.

Hata hivyo, ilisema katika ngazi ya sekondari masuala ya maadili hufundishwa katika somo la Civics kidato cha 1-4 na katika somo la General Studies kidato cha 5-6.

Masomo hayo ni ya lazima kwa wanafunzi wote wa sekondari huku ikisema masuala ya afya hufundishwa katika somo la biologia ambalo pia ni somo la lazima kwa wanafunzi wote wa kidato cha 1-4.

Pia ilisema serikali inaendelea na zoezi la kuboresha mitaala kwa ngazi ya Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari ambapo wanapokea maoni ya wadau ambayo yatazingatiwa katika maboresho ili kuhakikisha mitaala yetu inakidhi mahitaji ya inawajengea wanafunzi maadili ya kitanzania.

ALHAMISI SEPTEMBA 9, 2021

AFYA NA MAZINGIRA


Ukurasa 12

**Mabingwa waibua mapinduzi ya tiba kisasa kupitia vipimo vya vinasaba**


Ukurasa 14

**NEMC 'yaumiza kichwa' mbadala wa zebaki kunusuru afya za wachimbaji**

# Kliniki ya matembezi iko rasmi kuwafikia wagonjwa mafichoni

**Na Yasmine Protace**

KLINIKI tembezi ni moja ya mafanikio ya kitaifa katika sekta ya afya yanayomuwezesha mgonjwa aliyeko nyumbani, kufikiwa na matibabu aliko.

Ujumla wake ni kliniki mkombozi hata mjamzito anapopata uchungu ghafla anaweza kupatiwa msaada kupitia nyezo hiyo.

Kuanzishwa kliniki ya matembezi, kunatajwa kusaidia kuwafikia wagonjwa majumbani na sasa inatarajiwa matarajio kwamba, kliniki tembezi itasaidia kupunguza idadi au kuondoa kabisa wagonjwa wasiofikiwa au kuugulia majumbani.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema katika uzinduzi wa magari manne ya kliniki tembezi ya kisasa, pikipiki 160, mashine 50 na mamia ya mashine mbalimbali za tiba, jumla zikiwa na thamani ya shilingi billioni 6.2.

Anasema vifaa hivyo vilivyozinduliwa vitasaidia ama kupunguza idadi au kuondoa kabisa wagonjwa, wasiofikiwa wanaougulia majumbani nchini, katika hafla ya uzinduzi, Dk. Gwajima, aliufanya katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma.

Ni uzinduzi uliohudhuriwa na baadhi ya viongozi ngazi ya wizara na mkoa, lengo ni kuboresha huduma za matibabu ya kifua kikuu na ukoma, ili kuutokomeza nchini.



Pikipiki zitakazotumiwa na wataalamu wa afya katika kuwezesha huduma za kliniki tembezi. **PICHA: YASMINE PROTACE.**

"Jumla ya shilingi bilioni 6.2 zimetumika kununua magari haya ya kliniki tembezi na vifaa vya kutoa huduma za afya. Kiasi hiki ni kikubwa, sina budi kuwapongeza watumishi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma, kwa kufanikisha zoezi hili" anatamka.

Waziri anarejea kwamba, takwimu za mwaka jana, Tanzania ilikadiriwa kuwa na wagonjwa 135,000 na kati ya hao waliofanikiwa kubainiwa na kuwekwa kwenye matibabu, walikuwa 85,597 sawa na asilimia 63.

Waziri Dk. Gwajima, anasisitiza Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 duniani zenye tatizo kubwa la kifua kikuu na takribani watu 26,800 walifariki katika kipindi cha mwaka 2020.

Anasema licha ya jitihada zinazofanywa na wizara husika kufikia malengo ya kutokomeza maradhi hayo nchini, kunahitajika nguvu ya ziada kuwafikia na kuwaibua wagonjwa takribani 49,403, ambao hawakuweza kuwaibaini na bado wanaendelea kuambukiza ugonjwa huo katika jamii yetu.

"Takribani watu 26,800 walifariki katika kipindi cha mwaka 2020. Licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na wizara katika kufikia malengo ya kutokomeza kifua kikuu nchini," anasema na kusisitiza:

"Bado tunahitaji nguvu ya ziada kuweza kuwafikia na kuwaibua wagonjwa takribani 49,403, ambao hatukuweza kuwaibaini na bado wanaendelea kuambukiza ugonjwa huo katika jamii yetu."

Dk. Gwajima anasema dhima ya wizara yake ni kutokomeza kifua kikuu nchini kwa makundi maalum yanayotambulika katika ngazi ya jamii, kwa njia ya ushirikishwaji katika mapambano hayo.

"Dhima ya wizara ni kutokomeza kifua kikuu nchini, hivyo basi wizara imebuni mikakati mahususi, kwa ajili ya kuifikia jamii ambapo inajumuisha, kutumia kliniki tembezi, kwa ajili ya huduma mkoba za uchunguzi na ugunduzi wa kifua kikuu," anasema.

Anaendelea: "Kuongeza wigo wa mtandao wa maabara kwa kutumia teknolojia ya mashine za 'Gene Xpert' pamoja na kuimarisha mfumo wa 'lojistiki' katika uratibu na ufuatiliaji wa huduma hizo ngazi ya jamii na halmashauri kwa kutumia pikipiki.'

Dk. Gwajima anasema kliniki tembezi, pamoja na vifaa vinavyozinduliwa ni kielelezo cha utayari kufikia malengo ya kitaifa na dunia, huku akibainisha kliniki hizo zimefungiwa vifaa muhimu.

Anazitaja baadhi ya vifaa hivyo ni 'x-ray' za kidigitali na mashine anazotambulisha kwa jina 'gene xpert' ambazo ni teknolojia za kisasa zitakazoweza kuibua wagonjwa walioko katika maeneo, ambako huduma hizo hazipatikani.

**KWA WATAALAMU**

Dk. Gwajima anatoa rai kwa watumishi watakao endesha kliniki hizo kufanya kazi kwa weledi, kuzitunza na kuzijali kwani gharama iliyotumika ni kubwa, pia matengenezo yake ni ghali.

"Kliniki tembezi hizi zitagawanywa katika Hospitali za Kanda ikiwam ,Bugando (Kanda ya Ziwa), Hospitali ya Rufani ya Mkoa Dodoma (Kanda ya Kati), Hospitali ya Rufani Kanda ya Mbeya (Kanda Nyanda za Juu Kusini) na Maabara Kuu ya Kifua Kikuu iliyopo Dar es Salaam (Kanda ya Mashariki) na usimamizi wake utaratibiwa na hospitali hizo kwa kushirikiana na wizara," anasema.

Kuhusu pikipiki, Dk. Gwajima anaeleza matarajio yake ni kumaliza tatizo la waratibu kushindwa kutekeleza kikamilifu majukumu yao ya uratibu wa kifua kikuu na ukoma.

Hapo anataja majukumu kama usambazaji dawa na vifaa tiba, pia kusaidia kuwaibua wagonjwa wanaougua kifua kikuu na ukoma kwa kiwango kikubwa, hali kadhalika, itasaidia kipindi cha dharura wajawazito na wanaohitaji damu wakati wa uzazi.

AFYA

# Mabingwa waibua mapinduzi ya tiba kisasa kupitia vipimo vya vinasaba

## • Tabibu kupata uhakika kinachomsibu mgonjwa

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI kuna ukuaji wa teknolojia kwenye kila sekta ikiwamo afya, kunatajwa mapinduzi yanayokaribia nchini kwa vinasaba kutumika kama sampuli maabara, ili kuubaini ugonjwa kwa usahihi.

Wataalamu wa utafiti na vinasaba, wanasema kutokana na kuendelea kutumika teknolojia ya zamani, ambayo wadudu huoteshwa kuubaini ugonjwa, kumebainika yapo magonjwa yasiyogundulika kirahisi.

Katika nchi zilizoendelea matumizi ya vinasaba maabara yana muda, tofauti na nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, ambako kipimo anachopatiwa mgonjwa hospitalini kwa matibabu yaliyokithiri zaidi kwenye jamii, ni sampuli za damu, haja kubwa na ndogo

Makamu wa Rais wa Chama cha Watafiti na Wataaluma wa Vinasaba vya Binadamu Tanzania (THGO), Dk. Kilaza Samson, anasema upo uwezekano, tiba wanayopatiwa wagonjwa kadhaa isiwe sahihi, kwa sababu vipimo na sampuli zinazotumika kubaini magonjwa wanayougua, uwezo wake ni mdogo katika kutambua maradhi mengine.

"Kuna uwezekano kwamba tiba ambayo tunawapatia wagonjwa wetu isiwe sahihi, kwa sababu ya uchunguzi tunaoutumia ukitumia 'genetics' (vinasaba) unatoa vianasaba vya mgonjwa na kubaini kila kimelea katika sampuli na mgonjwa kupata tiba sahihi," anasema Dk. Samson.

Mtaaluma Samson, anasema hivi sasa kuna magonjwa mengi ikiwamo yaliyo adimu na yasiyo na tiba rahisi, kwa sababu namna ya kuyatambua ni ngumu, huku wanaougua wakipatiwa tiba isiyoendana na uhalisia wa wanachougua.

"Kwa kutumia njia ya kawaida tunayopima sampuli baadhi ya magonjwa hayatambuliki, imefikia wakati jamii hudai mtu huyu karogwa, sababu ana ugonjwa adimu ambao hugundulika kwa vinasaba tu,"



Rais Chama cha Watafiti na Wanataaluma ya Utafiti wa Vinasaba vya Binadamu Tanzania (THGO) Dk. Siana Nkya alipozungumza na wanahabari hivi karibuni, jijini Dar es Salaam. Kulia, ni Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto wa Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui na Katibu Mkuu THGO, Mohamed Zahir. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

### UTAFITI WAJA

Anasema kwa mara ya kwanza utafanyika utafiti, ambao utalenga makabila makubwa kuwakilisha mengine, ikizingatiwa Tanzania inayo takribani 120.

"Ingawa utafiti huu hauwezi kuyafikia makabila yote Tanzania yanafika kama 150, tutachukua sampuli kwa makabila machache, ambayo makubwa kwenye kanda za nchi kuwakilisha wengine. Hii itasaidia wanaougua kwenye mazingira kanda hii, kwa sababu gani, vinasaba vitagundua," anasema Dk. Samson.

Anafafanua kuwa, utafiti unaofanywa na vyuo vya tiba vikijikita kupata mafunzo ya kutumia vinasaba, utasaidia kulinda kizazi kijacho, akisema maradhi kama kisukari, presha ni kati ya magonjwa yanayo husiana zaidi na vinasaba.

"Tukijua uhalisia wa binadamu kwa kutumia vinasaba tutajua picha halisi na uasili wa kila alicho nacho binadamu hasa kiafya. Ndio maana, tunaweza kwenda hospitali wote tuna malaria, mmoja akapona na mwingine asipone na wote tumetumia dawa," anabainisha Dk. Samson.

Anasema vinasaba hugundua bakteria alio nao binadamu, walio wazuri waliopo tumboni, ambao bila kuwagundua kwa kutumia vinasaba, mgonjwa akipewa dawa isiyofaa huua wadudu hao walinzi.

### VINASABA VS TIBA

Profesa Raphael Sangeda kutoka Chuo cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), anasema ni kawaida kwa mtabibu kumhoji mgonjwa iwapo mmoja wa familia yao ana historia ya ugonjwa wa sukari, pumu au shinikizo la damu.

Anasema udodosaji huo, unalenga kubaini iwapo mhusika anaweza kuwa na tatizo, ambalo linatokana na urithi. Profesa Sangeda anafafanua:

"Japo elimu hii imekuwapo kwa matabibu na wataalamu wa afya kwa enzi na enzi, elimu na taaluma ya vinasaba vya urithi na changamoto zake kwenye magonjwa, bado ni finyu na ihahitaji kuendelezwa.

"Hivyo, tunashukuru THGO (Chama cha Watafiti na Wataaluma wa Vinasaba vya Binadamu Tanzania) na AsHG kuleta kongamano hili la vinasaba vya urithi, ili kutuweka Tanzania kwenye ramani ya dunia kama wadau wa kudhibiti magonjwa ya binadamu, kwa kuchunguza vinasaba husika."

Kuhusu taaluma ya vinasaba, anataja umuhimu wake katika kada za watoa huduma ya afya kama vile madaktari tiba na meno, wauguzi, wafamasia, matabibu meno, wataalamu wa maabara, wataalamu afya na wadau wengine.

Profesa Sangeda, anasistiza elimu hiyo ni muhimu kwa wanajamii wenyewe na waandishi wa habari, akiwa na angalizo la ziada:

"Japo matabibu wanao ufahamu wa magonjwa ya kurithi, wanahitaji kupata elimu zaidi na mafunzo juu ya vinasaba vya binadamu na jinsi ya kutumia hii elimu, kuboresha ugunduzi wa magonjwa na kutoa tiba sahihi, inayoendana na mpangilio wa vinasaba uliotofautiana kwa binadamu mmoja hadi mwingine.

"Kikemia, vinasaba hivi vinatengezwa na kemikali nne tu aina ya ACTG, lakini mpangilio wake ni tofauti kwa kila binadamu, mtiririko na mpangilio huo upatazo bilioni 30, ndio msingi wa kuboresha matibabu na ugunduzi wa magonjwa.

"Kwa hiyo mitaala ya elimu inahitajika katika vyuo vyetu kuwaelimisha wana-taaluma na wadau wengine juu ya mambo mbali mbali yanayohusu elimu ya vinasaba na afya."



Iilivyo umbo la jenetikia linalobeba chembehai za vinasaba.

### PENYE HITAJI

Profesa Sangeda anataja maeneo ambako mitaala inahitajika ni katika utumiaji vifaa tiba vya teknolojia ya kisasa ya kubaini mpangilio wa vinasaba vya binadamu, uchambuzi na uchakataji wa kanzidata na kumbukumbu za taarifa za wagonjwa pamoja na vinasaba.

Pia, anasema kunahitajika kubaini na kufahamu elimu ya urithi wa vinasaba ya maadili na sheria na masuala ya jamii .

"Msaada unahitajika kwenye kuandaa mitaala, kudahili wakufunzi, kutambua kada katika ikama ya serikali na kufuatilia ubora wa utoaji wa elimu hiyo. Waandishi wa habari wanalo jukumu la kuhakikisha kuwa jamii inapata uelewa mzuri juu ya vinasaba na uhusiano na magonjwa.

"Hii itasaidia wataalamu kupokelewa vizuri kwa mfano pale wanapoenda kufanya utafiti wa vinasaba vya makabila wakilishi ya Tanzania."

### MKUTANO KIMATAIFA

Rais wa chama hicho, Dk. Siana Nkya anasema Tanzania imeingia kwenye historia ya dunia kwa kushiriki kwa mara ya kwanza katika maandalizi ya kongamano la kimataifa linalojumuisha watafiti na wanataaluma wa stadi za chemchembe za binadamu za urithi.

Anasema ni mkutano ulioandaliwa na chama hicho kwa kushirikiana na chama mama cha Wanataaluma na Watafiti wa Vinasaba vya Binadamu cha Tanzania (African Society of Human Genetics Organisation) na Mtandao wa Wanataaluma wa Vinasaba wa Afrika (H3Africa), ukishirikisha wajumbe zaidi ya 300 kutoka duniani kote.

"Mkutano huu unashirikisha wadau wa nyanja mbalimbali za tafiti za vinasaba, wakiwamo wanafunzi wa digrii za uzamili na uzamivu, watafiti wachanga na wabobezi.

"Utafanyika uzinduzi wa jarida utafanywa na watafiti wabobezi Afrika akiwamo Profesa Julie Makani wa Tanzania, Profesa Wonkam (South Africa/Cameroon), Dk. Martin Mwangi (Malawi), Profesa Jackson Oryem (Uganda), na Dk Yvonne Dei Adomakoh (Ghana)."

"Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Serikali ya Jamuhuri ya Tanzania, Taasisi za kiserikali kama NIMR, Mkemia Mkuu wa Serikali, chuo kikuu na MUHAS, taasisi za kimataifa kama National Institute of Health, 54gene na Inqaba kwa kufadhili kongamano hili.

### UTAFITI UNAVYOTUMIKA

Mchakata vinasaba, Samson, aliyezama kielimu ngazi daktari wa falsafa, pia Makamu wa Rais wa THGO), anasema kutokana na dunia kupiga hatua kwenye teknolojia ya utafiti magonjwa, ni wakati Tanzania kujikita katika vinasaba.

Dk. Samson, Makamu wa Rais wa THGO anasema nchi zilizoendelea zilianza muda mrefu kuchunguza wagonjwa kwa kuhusisha teknolojia ya vinasaba, ili kubaini magonjwa kwa usahihi.

"Mfano mtu kafikishwa hospitali anaharisha, ukichukua sampuli maabara kwa kinyesi wataota wadudu, ila utaalamu wa sasa umebainisha kupima kwa njia hii kunaonyesha tunakosa asilimia 99 ya wadudu, ambao wapo kwenye kipimo hiki

"Kwanini? Kwa sababu, wadudu wengi hatuwafahamu, kwa kuwa hatuwafahamu hatujui tutumie virutubisho gani tuwaoteshe na kuwatambua. Kwa vipimo vya sasa, wadudu wanaoota ni wale ambao wanatambulika, kwa hiyo tunawakosa." Mtaalamu wa Vinasaba kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Ally Kanenda, anasema wamekuwa wakitumia teknolojia hiyo hususan kwa hitaji la jinai, migogoro na kubaini jinsi tata.

"Katika jinsi tata inarahisishia madaktari kuamua wanaozaliwa na jinsi tata wafanyiwe tiba na kubaki na jinsia moja. Tutashirikiana katika utafiti huu na chama hiki, ili kupata kanzidata ambayo haipo nchini," anahitimisha mtaalamu Kanenda.

AFYA

### MRADI WA MIAKA 25 KILOSA…

# World Vision yaondoka ikijivunia kudhibiti 'mlipuko' mimba utotoni

## • Bosi Mkuu amkabidhi kijiti DC 'kazi bado'
## • Wananchi: Tumebadilika, mimba 'kiduchu'

**Na Christina Haule, Morogoro**

KAMA ilivyo katika sehemu nyingine, wilayani Kilosa mkoani Morogoro nako wanalalamika mimba za utotoni, pia hata vifo. Ni balaa!

Hivi sasa kuna maoni Halmashauri Wilaya Kilosa, ikitakiwa kulivalia njuga suala la watoto kuolewa na kupata mimba katika umri mdogo, jambo linalochangia vifo vya wazazi wanapojifungua.

Lingine katika orodha hiyo, kuna suala la wanafunzi kukatisha masomo, hata kuvunja ndoto zao za maendeleo.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la World Vision Tanzania, Gilbert Kamanga, anasema wakati mradi huo ulianza mwaka 1996, kulikuwapo shida kubwa ya watoto wenye umri hata chini ya miaka 12, wakiolewa, hali inayochangia kundi kubwa la wanaoacha masomo kwa kutomaliza shule.

Ni kauli yake Kamanga, katika hafla ya shirika hilo lilipoagana na wananchi kumaliza mradi wake unaoitwa Magole ADP unaofadhiliwa na Wamarekani, ukitimiza mwaka wa 25 sasa.

Hafla hiyo ilifanyika kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Mgugu, iliyopo kwenye tarafa ya Magole wilayani Kilosa, huku Kamanga akikiri tatizo halijamazika katika baadhi ya maeneo kwenye jamii hiyo.

"Kulikuwapo kesi kubwa za watoto kuozeshwa wakiwa na umri mdogo wa chini ya miaka 12, lakini tumefanya kazi kubwa kuelimisha. Kundi la waelimishaji 60 kutoka kata sita za Tarafa ya Magole," anasema.

Rai yake kwa Mkuu wa Wilaya Majid Mwanga, ni kwamba, wahakikishe watoto wao wanamaliza shule kuondoa mimba za utotoni na anaishukuru serikali kwa kuonyesha utayari wa kufanya kazi na World Vision.

**DC KILOSA**

Mkuu wa Wilaya, Majid Mwanga, ametumia fursa hiyo kuwaagiza watendaji kata, akiwataka kutoa taarifa za kila wiki kuhusu watoto wasiokwenda shule na wanaopewa mimba, ili serikali iwachukulikie hatua wazazi wao.

Mwanga anaiasa jamii kuacha kuficha maovu yanayofanywa kwa watoto, akikumbusha mabinti ndio wenye huruma na walezi wakuu wa baadae wa jamii, akitoa mfano, familia kuwa na binti ni faida maradufu.

Mkuu wa Wilaya anatahadharisha, kuwa wazazi wanaoshirikiana na baadhi ya viongozi, haya kukwepesha kufuatilia mimba za mabinti, kwa visingizio vyenye hoja duni.

"Mtendaji wa kata na kijiji usicheke na anayempa mimba mwanafunzi, wakati wewe hukuharibu elimu yao hadi ulipofika na kazi yako na huchukui hatua inayostahili," anatahadharisha kwa angalizo la ukali:

"Nitakuchukulia hatua mimi! Haina maana kama kata moja pekee ya Mamboya kunakuwa na watoto 12 waliopewa mimba kwa mwezi mmoja. Hii ni aibu 'nitadili' na nyie watendaji kwanza na baadae wazazi."

Pia, anahamia kwa mabinti wanafunzi kwa sauti ya upole, huku akijitambulisha kuwa mzazi wao, anawataka wawe na juhudi masomoni na makini dhidi ya wanaume walaghai wanaojaribu kuwasogelea na daima atawalinda na kuwatetea.

Mkuu wa Wilaya anawageukia wavulana shuleni, akiwataka wawalinde dada zao wasiharibiwe na wavulana, huku akiwa mahsusi kwa waendesha bodaboda, ambao wanatawaja kuwa waharibifu wakubwa.

Kwa mujibu wa mkuu wa wilaya, dira iliyoko ni kuwafanya wanafunzi washindane wenyewe katika kuongeza ufaulu darasani na mitihani yao.

Anasema wapo madereva bodaboda na vijana wanaowaona wanafunzi kuwa sehemu ya kujifunza kwa vitendo, jambo ambalo halina maana kwa maendeleo ya wanafunzi, pia hata kwao.

**WANANCHI WANAHARAKATI**

Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi wa Mtoto kwenye Tafara ya Magole, kutoka kikundi cha Tupendane Priscar Chipela, anasema kuna jumla ya watoto 10 wenye umri chini ya miaka 18 waliopoteza maisha wakati wa kujifungua mwaka 1996.

Priscar anakiri watoto hao walifariki ni kutoka kundi la dunia la watoto 90 waliopata mimba wakati huo tajwa, wakati mradi ulikuwa unaanza.

Anasema kabla ya kuanza mradi wa Magole ADP, watoto waliishi mazingira magumu na hawakushirikishwa kwenye maamuzi yoyote kifamilia, wazazi waliozesha watoto wa umri wa chini ya miaka 18 na kusababishia kupata mimba za utotoni na kuwapo na vifo vingi vya watoto wakati wa kujifungua.

Priscar anaishukuru World Vision kwa kuwapa mafunzo wanachama 60 wa kamati ya ulinzi wa mtoto na kurejea vijiji vilivyopo kwenye kata sita za Tarafa ya Magole wilayani Kilosa.

Anazitaja kata sita zilizopata mafunzo hayo kuwa ni Kata ya Berega, Mamboya, Magubike, Mabula, Maguha na Mtumbatu, ambako kila kata wametoka watu 10 na kwenda kutoa elimu hiyo kwenye maeneo ya shule, misikiti, makanisa na mikutano inayoonekana kuzaa matunda.

Priscar anasema hivi sasa wanaendela kutoa elimu kwa jamii na kwamba hadi mwaka uliopo, ni mtoto mmoja ndiye alipata mimba kwenye umri chini ya miaka 18.

"Huwa tunatenga muda kwa kila wiki na mwezi na kutumia mikusanyiko mbalimbali, tunatoa elimu ya ulinzi wa mtoto na kufanya jamii kuanza kubadilika" anasema.

Mmoja wa wazazi, Rehema Changwala, anasema watoto katika maeneo hayo walikuwa wakiolewa wakiwa na umri mdogo, kutokana na matatizo ya umaskini na maisha duni ya wazazi wao.

Rehema, ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Magela, Kata ya Mabula, Kilosa anasema elimu waliyoipata kupitia World Vision, imewasaidia hasa walipoelimishwa kwenye kilimo na ufugaji wa kisasa.

Inatajwa kuwa katika orodha inayowaingizia kipato na kuwapunguzia umaskini unaowasukuma wanaume kukimbilia kupokea mahari, ili kuwezesha kujikimu, akisema miradi ya World Vision inawawezesha kujikimu na kubadilika kuacha tamaa ya fedha za kuwaozesha mabinti wadogo.

"Zamani mtoto akiwa na umri mdogo anapata mchumba na baba anachukua 'chake' mapema, ukeketaji vyote vilikuwapo, lakini tunaishukuru miradi ya Magole ADP," anaeleza.

Anakiri wamebadilika kwa kujikita zaidi kwenye kilimo cha kisasa kikiwamo cha mbaazi, mahindi, mboga na matunda yanayowasaidia kujikimu kimaisha.

Mzee Stumaini Mnyanda, mkazi wa Kijiji cha Msalama Berega, anawataka wazazi wenzake kushikilia maagizo na mitazamo ya World Vision wa kutoozesha watoto katika umri mdogo.




Asasi ya World Vision, ilipohudumia miradi tofauti wilayani Kilosa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



MAZINGIRA

# NEMC 'yaumiza kichwa' mbadala wa zebaki kunusuru afya za wachimbaji

## • Mimea na mazingira nayo njia panda

**Na Joseph Mwendapole**

MATUMIZI ya zebaki kwa wachimbaji madini wadogo ni hatari kwa maisha yao ya kawaida, hata kuathiri afya za baadhi yao, huku ikiharibu mazingira kwa ujumla, pale isipotumika kwa makini.

Inapotumiwa bila ya uangalifu, mabaki ya kawaida ya zebaki yanaposambaa kwenye mazingira ya kawaida, inamuachia madhara makubwa ya kiafya binadamu.

Kwa kuliona hilo, Mamlaka ya Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC), imeandaa utafiti kuwapa mbadala unaowawezesha wachimbaji wadogo kufanya shughuli zao za kila siku kuwaingiza kipato, pasipo athari za mazingira.

Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Zebaki, kwenye uchimbaji mdogo wa dhahabu nchini, Mhandisi Benjamin Mchwampaka, ameiambia Nipashe, kuwa kuna madhara mengi ya kemikali hiyo, hivyo wana mipango ya kutafuta mbadala sahihi.

Anasema, Tanzania inakadiriwa kuwa na wachimbaji wadogo wa madini milioni mbili, hivyo si rahisi kusitisha matumizi ya zebaki, ili kunusuru ajira na uchumi wa mamilioni ya Watanzania

Hata hivyo, kuna mbadala wa kuokoa mazingira na viumbe hai. Anasema lengo la dunia ni kupunguza au kutokomeza kabisa matumizi ya zebaki.

Ila nchini, anasema wanaona suluhisho ni kutafiti na kupata mbadala wake kwanza, kabla hatua ya kudhibiti matumizi ya kemikali hiyo kwanza.

Anasema, mradi huo utakaokuwa wa miaka mitano, unasimamiwa na NEMC na kutekelezwa kwenye mikoa ya kipaumbele wanakopatikana wachimbaji wengi wa dhahabu; Geita, Mwanza, Mara, Shinyanga, Singida, Mbeya na Songwe.

Mhandisi Mchwampaka, anasema iwapo matokeo kwenye mikoa hiyo yatakuwa mazuri, basi mradi utaenda kwenye mikoa mingine, lakini kwa sasa NEMC imetoa kipaumbele huko, kwa sababu ya wingi wa wachimbaji wadogo.

Anasema zebaki ni kemikali yenye matumizi mengi, lakini wachimbaji wadogo wanaitumia kuzalisha dhahabu kutoka kwenye miamba na wanapomaliza kusaga mwamba wakapata unga, wanaosha na kuweka zebaki, ili kunasa dhahabu kutoka kwenye udongo.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira (NEMC), Dk Samuel Gwamaka, alipozungumza kwenye moja ya mikutano

"Dhahabu ikiwa tayari, wanaenda kuchoma na zebaki inaondoka kama mvuke na hapo ndipo dhahabu inapopatikana na kupelekwa sokoni. Kwa wachimbaji wadogo hiyo ni njia rahisi kwao ndiyo maana wanaipenda," anasema Mhandisi

Ila anatoa angalizo kwamba madhara ya kemikali hiyo ni makubwa sana kwa afya ya binadamu na viumbe hai iwapo itasambaa na kwenda kwenye mito, bahari au vyanzo mbalimbali vya maji

Mchwampaka anasema, zebaki inaposambaa inaweza kuliwa na viumbe wadogo wanaliwa na samaki, wanapovuliwa na kuliwa jamii ina uwezekano mkubwa wa kupata madhara.

### JUKWAA LA MFANO

Mfano hai uko mwaka 1956, madhara yake yaligunduliwa katika kitongoji kinachoitwa Minamata Kusini mwa Japan, ambako jamii ya wavuvi walivua samaki wenye zebaki na baada ya muda mfupi, watoto wa jamii hiyo walionekana kupata magonjwa tata kwenye misuli, kushindwa kusimama na wapo walioshindwa kuongea

"Baada ya ugonjwa huu kujulikana, dunia ikaweka azimio kwamba madini haya yadhibitiwe, kwa sababu yanaleta madhara. Ndipo mwaka 2013, ukasainiwa mkataba maarufu unaoitwa Minamata na nchi 218, ikiwamo Tanzania na mwaka 2020 iliridhia kuanza kusimamia mkataba huo.



Wachimbaji wadogo wa madini, ambao pia ni watumiaji wakubwa wa zebaki, wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Anasema, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), iliunda mpango mkakati wa kutekeleza azimio hilo, hasa katika kipengele kinachoeleza namna nchi inapaswa kuweka mkakati wa kupunguza au kuondoa kabisa matumizi ya zebaki

"Ndio mradi huu sasa ambao NEMC inautekeleza, wataalamu tulikaa tukaandika tukaomba fedha Benki ya Dunia na Shirika la Global Environmental Facility lilikubali kufadhili mradi huu kwa jumla ya Dola za Marekani 7, 339, 450," anasema

Kwa mujibu wa Mchwampaka, maandalizi yameshakamilika na wamefungua akaunti za kuingiza fedha za mradi huo mwaka huu na kuanza kufanya kazi, kuhakikisha wachimbaji wadogo wanazalisha dhahabu kwa kutumia mbadala, mbali na zebaki.

Anasema, wataangalia maeneo yaliyoharibiwa na wachimbaji wadogo kwa kukata miti na kuacha mashimo wazi, warudishe mazingira hayo yawe kama ilivyokuwa awali.

Pia, ana ufafanuzi kuwa mradi huo una maabara nne: Mkemia Mkuu wa Serikali, NEMC, Tume ya Madini na Wakala wa Jiolojia Tanzania, zitakazo ongezewa uwezo wa kununua vifaaa vyenye uwezo zaidi, kupima madhara kwenye hewa, ardhi na majini

Anasema, kwa sasa mradi upo kwenye utekelezaji zaidi na kwa kiwango kikubwa unalenga kuwaelimisha wachimbaji wadogo, wanapokamata dhahabu kwa kutumia zebaki wakati uliopo, ambao mbadala haujapatikana, wanapaswa kutumia vifaa kinga.

"Unakuta mwanamke anakaamatisha dhahabu kwa kutumia zebaki, lakini hana vifaa vya kujikinga kwenye mikono yake na akitoka hapo, labda anakwenda kunyonyesha mtoto. Sasa dhahabu kwa bahati mbaya ikimwingia mtoto, ni hatari kubwa," anatahadharisha

Anasema, ni rahisi sana zebaki kuharibu mfumo wa fahamu mwilini, figo zinakufa na wanawake wenye mimba wanaweza kuathiri mimba ama kutoka au madhara, kama kuzaliwa watoto taahira na kwamba maradhi yaanarithishwa kutoka uzao mmoja kwenda mwingine

Mtaalamu huyo anatumia mfano, kwa maana athari inaweza kuhama kutoka mzazi hadi mjukuu kuzaliwa na ama ulemavu au athari katika mfumo wake wa ufahamu.

Anarejea kilichotokea nchini Japan, miongo mingi hadi sasa kuna baadhi ya watu wanaendelea kudhurika, kutokana na athari za babu na bibi zao, kabla ya kudhibitiwa.

### ZEBAKI NA MAZINGIRA

Inaelezwa, serikali pindi zebaki inaendelea kutumika bila kudhibitiwa, inapofika kwenye mito na maziwa,. Ni hatari nyingine ya kupoteza fursa ya utajiri wa samaki watakaokufa.

Anasema, ni vyema kuendelezwa mikakati ya kuidhibiti, ili kulinda mito na samaki nchini, ambao ni lishe na utajiri wa fedha za kigeni, ingawaje Mchwampaka anakili, si rahisi kudhibiti athari hiyo kwa asilia zote, kwani wachimbaji wadogo wanaegemea mfumo huo wa uchimbaji dhahabu kwa uchumi wao.

"Ndiyo maana tunakwenda taratibu, kwa kuanza kutoa elimu, wakati tunatafuta njia mbadala. Sasa itakapopatikana na wachimbaji wadogo wakiwa wameifahamu, tutakuwa na haki ya kuizuia, ila kwa sasa haiwezekani kuizuia isiingie nchini," anaeleza

Anaeleza kuwa hadi sasa, wamesha waainisha wataalamu na njia rahisi, zenye gharama nafuu kutumia mbinu hizo



# Wataalamu kusaka mwafaka na TLTC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo kwa kushirikiana na kampuni ya ununuzi wa tumbaku (TLTC), imeunda timu ya wataalamu kwa ajili ya kutafuta mwafaka baada ya kampuni hiyo kusitisha shughuli zake nchini mwaka 2018.

TLTC ni kampuni tanzu iliyo chini ya kampuni ya Universal ambapo nchini ilianza rasmi shughuli zake mwaka 1997 baada ya kununua mitambo ya uchakataji wa tumbaku iliyokuwa inamilikiwa na serikali kupitia kampuni ya TTPL.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, aliyasema hayo alipokuwa baada ya kikao chake na wawakilishi wa kampuni hiyo.

Alisema pamoja na timu hiyo kupitia hoja na kutafuta utatuzi, lakini kampuni hiyo inatakiwa kupitia maamuzi yake ya kusitisha shughuli zake nchini na kama kuna jambo wanataka liondolewe waliseme.

"Kampuni hii imekuwapo nchini kwa muda mrefu na ilikuwa inafanya kazi ya kununua tumbaku na mwaka 2018 waliamua kuacha kununua tumbaku na kufanya biashara Tanzania na baada ya wao kuondoka tulifanya nao kikao mwaka 2019 na kueleza mambo matano yanayowasumbua katika nchi yetu," alisema.

Alitaja mambo hayo kuwa ni adhabu za penati walizokuwa wamepigwa na FCC kama sekta nzima ya tumbaku, masuala ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), mazingira ya biashara.

"Katika kikao kilichofanyika mwaka 2020 chini ya aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ambapo yalijadiliwa mambo matano yaliyokuwa yakiathiri sekta ya tumbaku, tulifanyia kazi na kampuni nyingine ziliendelea na kuongeza uzalishaji na uliongezeka hadi kufikia tani 67,000 kutoka tani 37,000 hadi 40,000 za wakati huo," alisema.

Alisema serikali iliendelea na majadiliano na kampuni hiyo ili irudi nchini kuendelea na shughuli zake.

"Tumeanza majadiliano ya kikao cha kwanza, na serikali tumewauliza kwanini wanataka kuondoka, wakasema ni maamuzi ambayo wamefikia na tumewaambia maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha tunatatua changamoto zinazowakabili wakulima," alisema.

Alisema kikao cha pili kitafanyika Oktoba mwaka huu na kwamba kampuni hiyo ni muhimu kutokana na miundombinu waliyouziwa na serikali.

# Gwajima: Takwimu zenye ubora tatizo kwenye h'shauri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema matumizi ya takwimu zenye ubora katika halmashauri nchini bado ni kikwazo na zinarudisha nyuma sekta ya afya.

Dk. Gwajima aliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya kwanza ya wataalamu wa fani ya ufuatiliaji wa magonjwa kwa ufanisi na usimamizi wa maabara nchini yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema katika jamii ni lazima kuwapo na takwimu zenye ubora katika ngazi zote, jambo litakalosaidia kuinua sekta hiyo.

Aidha, alisema ni vyema kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa magonjwa na matukio yanayoathiri afya kwa kutambua mapema viashiria vya hatari.

Alitoa wito kwa idara na taasisi za serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kutambua umuhimu wa fani ya Epidemiolojia ili kutambuliwa kwenye mfumo wa utumishi wa umma.

"Kuna changamoto kubwa kwa wataalamu wa Epidemiolojia na maabara hapa nchini kutotambulika kwa kada hii kwenye mfumo wa ajira wa serikali," alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo itasaidia kutoa motisha kwa wataalamu hao na kupelekea kuongeza ufanisi katika utendaji

wao wa kazi.

Alisema watumishi 512 kutoka Idara ya Afya ya Binadamu na Afya ya Mifugo wamepatiwa mafunzo katika ngazi ya kozi ya awali kutoka katika mikoa yote 26 na

halmashauri 169 kwa kipindi cha miaka sita.

Naye Rais wa Chama cha Wataalamu wa Udhibiti na Ufuatiliaji wa Magonjwa Tanzania (TANFLEA), Elibariki Mwakapeje, aliishukuru wizara kwa kutilia mkazo juu ya kufanyika ufuatiliaji kwa kada ya wataalamu.



Kamishna Jenerali wa Idara ya Uhamiaji, Dk. Anna Makakala (kushoto), akijadiliana jambo na Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Johari Masoud Sururu (katikati), pamoja na Kamishna wa Uhamiaji Divisheni ya Sheria, Edmund Mrosso, walipokutana kwenye viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CSSC yataka kasi bima ya afya kwa watu wote

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuharakisha mchakato wa bima ya afya kwa wote ili kila Mtanzania apate matibabu ya uhakika anapougua.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kikristo ya Huduma za Kijamii (CSSC), Peter Maduki, aliyasema hayo kwenye Mkutano Mkuu wa 84 wa mwaka wa Chama cha Madaktari wa Kikristo Tanzania (TCMA), unaofanyika jijini hapa.

Alisema ni vyema serikali ikatekeleza kwa haraka mchakato huo ili kila Mtanzania awe na bima.

"Ili wananchi wote waweze kupata huduma bora tunaiomba serikali itekeleze bima ya afya kwa wote mara moja ili kusudi watoto, watu wazima na kinamama na watu wote waweze kunufaika," alisema.

Aidha, Maduki aliwahamasisha Watanzania kujiunga na bima ya afya kuanzia ile ya jamii na Taifa ili kupata huduma za afya.

"Nawahamasisha wananchi waweze kujiunga na bima ya afya kuanzia ngazi mbalimbali kuanzia ile ya jamii na ile ya taifa kuhakikisha wanapata huduma kwa wakati," alisema.

Alisema wao kama kanisa wanaendelea kuwaelimisha Watanzania kuendelea kupata chanjo ya UVIKO-19 na kwamba wameandaa mafunzo kwa wataalamu wa afya, jinsi ya kujikinga pamoja na kutoa vifaa (PPE) ambavyo wamevigawa katika hospitali 200 nchini.

"Kama kanisa tunapendekeza kwamba watu waweze kupata chanjo ndio maana sisi tumehakikisha tunatoa mafunzo kwa wataalamu wa afya waweze kujikinga pia tumehakikisha tunapata vifaa vya kutosha kutoka kwa wadau wetu na kuvigawa katika hospitali zetu zipatazo takribani 200," alisema.

Kadhalika, Maduki alisema wameendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wa dini ili wawe na uelewa wa kuelimisha waumini.

Hata hivyo, Maduki alisema katika mkutano huo watazungumzia namna bora ya kuboresha sekta ya afya, elimu pamoja na kuhamasisha matumizi ya bima ya afya ili Watanzania wengi wapate huduma pindi wanapougua.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Huduma za Afya CSSC, Dk. Josephine Balati, alisema Tume hiyo inajishughulisha na utoaji wa huduma za afya na elimu ambazo zinatolewa na makanisa nchini na wanafanya kazi na taasisi zaidi ya 900 ambazo zipo sehemu mbalimbali hapa nchini.

"Sisi ambao tunafanya kazi na hizi taasisi za dini tunashirikiana sana na serikali yetu. Katika chanjo tunashiriki kikamilifu kuielimisha jamii kuchanja tunajua ukubwa wa tatizo hili kwa hiyo tunaendelea kuihamasisha jamii kuchanja. Sisi tumeshirikiana na wadau kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi," alisema Dk. Balati.

Alisema suala la elimu bado linahitajika ambapo kwa kupitia taasisi zao wameendelea kuwahamasisha viongozi wa dini pamoja na kuwajengea uwezo ili jamii ione umuhimu wa kuchanja.





# Serikali yaiagiza TALIRI kutoa elimu kwa wafugaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeiagiza Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) Kituo cha Uyole, kuanza kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uandaaji wa malisho bora ili kupunguza migogoro baina yao na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na kuboresha mifugo yao.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kukagua vitalu vya utafiti wa malisho ya aina mbalimbali katika kituo hicho ambayo baadhi ni ya asili na mengine yameletwa nchini kutoka nchini China.

Alisema taasisi hiyo ina wajibu wa kuwasaidia wakulima kuandaa malisho yao wenyewe kwenye maeneo yao ili kuboresha mifugo yao pamoja na mazao yatokanayo na mifugo hiyo yakiwamo maziwa, nyama na ngozi.

Homera aliitaka Taasisi hiyo kusambaza malisho hayo kwa wafugaji baada ya kumaliza utafiti ili manufaa ya kituo hicho yaonekane kwenye jamii badala ya tafiti hizo kubaki kwenye makaratasi kama ambavyo imekuwa ikitokea kwenye taasisi zingine.

"Mkishamaliza utafiti wa malisho haya, andaeni taarifa ili tuipeleke kwa wafugaji, lakini pia mtoe elimu kwa wafugaji namna ya kuandaa malisho haya kwenye maeneo yao, hii itatusaidia kupunguza migogoro ya ardhi," alisema Homera.

Alisema halmashauri zinatakiwa kuwasaidia wafugaji kuandaa malisho hayo kwenye maeneo waliyotengewa ili kuepusha migogoro ya wafugaji na hifadhi za taifa pamoja na migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alizishauri pia halmashauri za mkoa huo kuwapeleka vijana wanaowezeshwa kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenye Taasisi hiyo ili vikajifunze namna ya kuandaa malisho hayo na kuyauza kwa wafugaji.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TALIRI, Dk. Edwin Chang'a, alisema wameamua kuanza utafiti wa malisho ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa malisho kwa wafugaji hasa kipindi cha kiangazi ambacho kunakuwa na tatizo la malisho.

Alisema wamekuwa wakiandaa malisho ya asili ambayo ni pamoja na mabaki ya mazao mbalimbali yakiwamo maharagwe ambayo alisema wamebaini kuwa yana protini nyingi zinazowezesha mifugo kustawi vizuri.

Pia, alisema yapo malisho mengine ambayo wamekuwa wakiyapanda na kuyavuna yajulikanayo kwa jina la 'Hey' ambayo yanaandaliwa na kufungwa kwenye mafungu.

"Kuna baadhi ya malisho hasa haya mabingombingo tulishaanza kuyasambaza kwa wafugaji hasa kule Rungwe ambako kuna tatizo kubwa la malisho na yameleta ufanisi mkubwa sana," alisema Dk. Chang'a.

Mkuu wa Idara ya Malisho wa Kituo hicho, Peter Nchimbi, alisema kwenye kituo hicho wanafanya utafiti wa malisho ya kisasa na ya asili ambayo baadhi yametolewa katika mataifa mbalimbali duniani na mengine yamechukuliwa nchini.

Alisema walikusanya malisho ya asili kutoka katika mikoa yote nchini mpaka sasa ni malisho ya kutoka katika mikoa 10 ndiyo yaliyobaki kuendelea kufanyiwa utafiti kulingana na kanda mbalimbali.

Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa inayokabiliwa na migogoro ya wakulima na wafugaji, wafugaji na hifadhi kutokana na uhaba wa malisho, hivyo endapo elimu ya malisho itatolewa kuna uwezekano migogoro hiyo ikaisha.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo nchini (TALIRI) Kituo cha Uyole, Dk. Edwin Chang'a, kuhusu utafiti wa malisho katika kituo hicho, jijini Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Marufuku kusafirisha petroli kwenye vidumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limepiga marufuku wananchi kusafirisha mafuta aina ya petroli kwa kutumia vifaa visivyokubalika kisheria ili kuepuka madhara ikiwamo mlipuko wa moto.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliyasema hayo juzi wakati alipokuwa anazungumza na waandisi wa habari kuhusu matukio mbalimbali ya uhalifu.

Alisema Jeshi hilo juzi usiku lilikamata gari moja aina ya Canter likisafirisha lita 2000 za petroli kwenye madumu ya lita 20 ambayo yalikuwa 100.

Alisema katika tukio hilo Jeshi hilo liliwakamata vijana wawili, Medrisa Yohana (21), mkazi wa Mji wa Mbalizi na Hussein Nyoni ambao walikuwa wanasafirisha bidhaa hiyo na haijulikani mafuta hayo waliyachukua wapi.

"Sisi kwa hatua za awali hatuhangaiki na uhalali wa mafuta haya, lakini tunahangaika na usafirishaji, hii ni hatari sana maana haya yakipata moto hapa yanaweza kulipuka na kuleta madhara, sasa hivi nataka hata hapa waliondowe gari hili hapa," alisema Kamanda Matei.

Alisema matukio ya moto yamekuwa yakitokea mara nyingi kutokana na uzembe wa wananchi hasa kwenye utunzaji wa mafuta hayo ambayo aliyaita kuwa ni sawa na 'vilipuzi'.

Alisema kwa mtu yeyote anayetaka kusafirisha mafuta hayo anatakiwa kutumia magari maalumu ya kusafirishia yajulikanayo kwa jina la 'Tanker'.

# TRA yapata mafanikio ukusanyaji kodi kwa mazungumzo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema utaratibu wa kukusanya kodi kwa njia ya mazungumzo na walipakodi umekuwa na manufaa kwenye makusanyo kuliko utaratibu wa awali ambao walikuwa wanatumia vikosi maalumu vijulikanavyo kama 'Task Force'.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi kutoka TRA Makao Makuu, Richard Kayombo, aliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa kutoa elimu kwa waandishi wa habari wa kuhusu mabadiliko mbalimbali ya sheria.

Alisema utaratibu huo umesaidia kurahisisha ukusanyaji wa mapato na umewafanya wananchi wengi kuanza kulipa kodi kwa hiyari bila kulazimishwa.

Alisema pia uliisaidia Mamlaka hiyo kuongeza ukusanyaji kuanzia mwezi Aprili mpaka sasa na wanatarajia kukusanya fedha nyingi zaidi mwezi Septemba ambao alisema ni mwezi mrefu zaidi.

Alisema walipakodi wanajitokeza kwa wingi kwenye ofisi za mamlaka hiyo kwa ajili ya kujadiliana na kukubaliana namna ya kulipa madeni na malimbikizo ya kodi na baada ya kukubaliana wanalipa kwa awamu.

Alisema pamoja na kuutumia utaratibu huo, Mamlaka hiyo itaendelea kutumia mbinu zingine kwa walipakodi ambao wanakiuka makubaliano na kwamba hatua ya kufunga akaunti za benki ni hatua ya mwisho kwenye zoezi hilo.

Aliwataka walipakodi waendelee kujitolea kulipa bila kulazimishwa na kwamba serikali itaendelea kuwahudumia kwa kurejesha baadhi ya fedha hizo kwa wananchi kwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Ofisa Msimamizi wa Kodi, Idara ya Elimu na Huduma kwa mlipa Kodi kutoka TRA, Isihaka Sharif, aliwataka walipakodi kuhakikisha wanatunza vizuri kumbukumbu za ulipaji wao ili kuepuka migogoro ambayo haina tija.

Alisema wafanyabiashara wote wanatakiwa kuhakikisha wanatoa risiti kila wanapouza bidhaa huku akiwataka wananchi kutoa taarifa pale wanapobaini baadhi ya wafanyabiashara wakikwepa kodi kwa kutotoa risiti.

Alisema kila Mtanzania anatakiwa ashiriki kwenye ukusanyaji wa mapato na anayenunua alipe, adai risiti na anayeuza atoe risiti.

"Wale wanaotumia Mashine za Kielektroniki (EFDs) wahakikishe anatumia karatasi zenye ubora ili taarifa zionekane, yamekuwapo malalamiko ya baadhi ya wananchi kwamba risiti hizo huwa zinafutika," alisema Sharif.

Baadhi ya wanahabari waliohudhuria mafunzo hayo, waliuomba uongozi wa TRA kuendelea kutoa elimu hiyo ili kuwarahisishia kufikisha taarifa kwa wananchi zinazohusu kodi.



# Wizara yaanza utafiti mbegu za matunda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili na Umwagiliaji, imesema imeanza kufanya utafiti wa mbegu za mazao ya kilimo na matunda kwa ajili ya kilimo chenye tija na kuwakomboa wakulima.

Hayo yalisemwa jana na Waziri Dk. Soud Nahoda, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Kombo Mwinyishehe, aliyetaka kujua juhudi zinazochukuliwa na wizara katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwamo cha matunda na mizizi.

Dk. Nahoda alisema baadhi ya mbegu zimeshafanyiwa utafiti na kugaiwa kwa wakulima ikiwamo za muhogo mbegu aina ya Machuwi, Kizimbani ambazo zimeonyesha mafanikio makubwa katika hatua za majaribio.

Alisema zipo mbegu zimefanyiwa majaribio za viazi vitamu ambazo ni nzuri na husaidia kutoa lishe kwa wananchi zimeanza kutumiwa na wakulima.

"Mheshimiwa Spika mbegu za majaribio tayari tumezipeleka kwa wakulima ambazo katika utafiti wa awali zimeonyesha matumaini makubwa ya kiwango cha uzalishaji," alisema.

Alisema mbegu za mpunga aina ya Super DC kwa mujibu wa utafiti uliofanywa wa majaribio yake katika kituo cha utafiti wa kilimo na mazao cha kizimbani unaonyesha uwezo mkubwa wa uzalishaji na kuleta tija kwa wakulima.

"Hii mbegu tumeifanyia utafiti na majaribio kwa wakulima mbalimbali ambayo inaonyesha ina uwezo wa kuzalisha mpunga tani saba kwa hekta moja," alisema.

**Hayo yalisemwa jana na Waziri Dk. Soud Nahoda, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Kombo Mwinyishehe, aliyetaka kujua juhudi zinazochukuliwa na wizara katika kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwamo cha matunda na mizizi.**

# Rais Mwinyi avunja Bodi ya Vileo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amevunja Bodi ya Ushauri ya udhibiti wa Vileo huku Mwanasheria Mkuu na Bodi hiyo, akifunguliwa mashtaka na Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) ya kuvunja sheria namba 9 ya mwaka 2020.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Injinia Zena Ahmed Said, imeeleza kuwa bodi hiyo imevunjwa na Rais kuanzia Septemba 7, mwaka huu.

"Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ameivunja bodi ya ushauri ya udhibiti vileo Zanzibar kuanzia Septemba 7, mwaka huu na ilikuwa chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum," alisema Zena katika taarifa yake.

Hata hivyo, akieleza sababu ya bodi hiyo kuvunjwa, lakini uamuzi huo umekuja huku Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar na Bodi ya Ushauri Udhibiti wa Vileo ikikabiliwa na kesi dhidi ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) kwa madai ya kuvunja Sheria namba 9 baada ya kutoa vibali kwa kampuni za kuingia vileo zaidi ya tatu kinyume na sheria.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo ya maombi katika kesi hiyo JUMAZ inadai kwa mujibu wa kifungu cha 33(1) kampuni tatu ndiyo zinatakiwa kupewa vibali vya kuingiza vileo.

Kifungu hicho kimefafanua kuwa "kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waagizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo mwingizaji awe Mzanzibari, awe mlipakodi mwenye ghala na gari ya kusambazia vinywaji hivyo.

JUMAZA pia inadai kifungu cha 28 (K) cha Sheria ya Bodi ya Ushauri ya Udhibiti wa Vileo imeweka masharti ya leseni za baa kupewa wamiliki kwa masharti ya baa iwe umbali wa mita 1000 kutoka maeneo ya huduma za jamii ikiwamo shule, nyumba za ibada, hospitali na makazi, lakini bodi imeshindwa kuzingatia masharti hayo.

Akizungumza kuhusu uamuzi wa Rais kuvivunja bodi, mwanaharakati wa haki za binadamu na utawala bora, Ali Makame Issa, alisema Rais anapaswa kupongezwa kutokana na uamuzi huo baada ya kuwapo malalamiko mengi katika jamii.

"Rais wetu anaonyesha ni mtu msikivu kero za wananchi anazifanyia kazi kwa vitendo kwa maslahi ya taifa na wananchi wake, tunampongeza sana kwa kusikiliza kilio hiki," alisema Makame.

Hata hivyo, Makame alisema viongozi wapya wa bodi watakaoteuliwa lazima waangalie watu wenye uwezo na wazalendo ambao watakuwa na uwezo wa kulinda sheria kwa maslahi ya taifa na wananchi wake.

Aidha, alisema mpango wa wanaharakati na viongozi wa madhehebu ya dini kufanya kongamano la pamoja na kuvunjwa sheria ya vileo Zanzibar sasa utategemea na bodi mpya itakavyosimamia sheria na uwajibikaji kwa maslahi ya taifa na wananchi.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (wapili kulia), akitoa maelekezo ya namna ya kuwasaidia wanafunzi wa fani ya mafuta na gesi kuingia katika soko la ajira, baada ya kufungua maabara za nishati mbadala, mafuta na gesi katika Chuo cha Taasisi ya Karume Sayansi na Teknolojia, Mbweni mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mahakama za udhalilishaji zasaidia kasi usikilizaji kesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema mahakama za udhalilishaji wa kijinsia zimeanza na zimesaidia kuongeza kasi ya kusikiliza kesi hizo na kutoa hukumu zake.

Suleiman alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa tiketi ya CCM, Machano Othman Said, aliyetaka kujua kuanza kwa mahakama za udhalilishaji wa kijinsia na mafanikio yake katika kipindi cha mwaka mmoja.

Akitoa ufafanuzi huo alisema kwa upande wa Zanzibar Mahakama za udhalilishaji wa kijinsia zipo katika mahakama ya Mwera, Vuga pamoja na Mahonda, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema kwa upande wa Pemba mahakama za udhalilishaji wa kijinsia zipo katika Wilaya ya Chakechake pamoja na mkoani Pemba.

Alizitaja juhudi zilizochukuliwa ambazo zimefanikisha kusikilizwa kwa haraka kesi za udhalilishaji wa kijinsia ni kuongezwa kwa idadi ya mahakimu na kwa upande wa Unguja wameteuliwa mahakimu wapya wanane na Pemba watatu.

Alisema katika ngazi za mikoa idadi ya watendaji wa Mkurugenzi wa Mashtaka DPP wameongezwa hatua ambayo imesaidia kuwapo kwa mafanikio ya kasi ya kesi za udhalilishaji wa kijinsia kutolewa hukumu.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga zaidi kuongeza kasi ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia ambapo kwa upande wa watendaji wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) tunakusudia kufanya ajira zaidi ya watumishi," alisema.

Suleiman aliwataka wananchi kuachana na muhali ambao ni chanzo cha kuchelewesha kusikilizwa kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia katika mahakama zote kiasi ya kesi kuchukua muda mrefu kusikilizwa.

"Muhali ni moja ya changamoto kubwa ambapo wakati mwingine kesi za udhalilishaji wa kijinsia hulazimika kufutwa mahakamani kwa sababu watu hawapo tayari kutoa ushahidi mbele ya mahakama kwa kuogopa lawama," alisema.

HABARI KIMATAIFA

## Wanafunzi wafukuzwa shule wakijirekodi picha ya ngono

**Kinshasa,** DRC

WANAFUNZI sita wa sekondari Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wamepigwa marufuku kuhudhuria shule yoyote katika taifa hilo, baada ya video ya ngono waliyoshiriki kusambaa mtandaoni.

Wanafunzi hao walifukuzwa shule na Waziri wa Elimu Tony Mwaba.

Video hiyo ilipigwa picha nje ya shule yao iliyopo mjini Kinshasa, ikiwaonesha wamevaa sare za shule.

Shule tano za wavulana na moja ya wasichana zilionekana kwenye video hiyo.

Waziri wa Haki za Binadamu, Albert-Fabrice Puela, alisema marufuku hiyo inaminya haki za watoto.

**BBC**

## Moto wateketeza wafungwa 41 gerezani

**Jakarta,** INDONESIA

WATU wapatao 41 wamekufa baada ya moto kutokea katika Gereza la Indonesia lililopo pembezoni mwa mji mkuu wa Jakarta.

Moto huo ulitokea majira ya asubuhi sana, jana, katika Gereza la Tangerang wakati wafungwa wengi wakiwa wamelala.

Kulikuwa na wafungwa 122 katika gereza ambalo liliathiriwa na moto.

Gereza lote lina wafungwa 2,000 idadi iliyozidi kiwango cha gereza hilo, ambacho ni watu 600.

Wafungwa hao wengi walikuwa wanashikiliwa kwa makosa ya kujihusisha na dawa za kulevya.

Watu kadhaa wanadaiwa kujeruhiwa wengine wakiwa kitengo cha wagonjwa mahututi.

Hitilafu ya umeme inadaiwa kuwa chanzo cha moto huo, alisema msemaji wa gereza hilo ingawa alieleza pia uchunguzi zaidi unafanyika.

**BBC**

## Watumishi Zimbabwe watakiwa kuchagua kazi ama chanjo

**Harare,** ZIMBABWE

SERIKALI ya Zimbabwe imewataka wafanyakazi wake kupata chanjo dhidi ya Covid-19 au waache kazi.

Inasema hatua hiyo inalenga kupunguza hatari ya kueneza virusi.

Katika mahojiano na kituo cha redio cha eneo hilo, Waziri wa Sheria Ziyambi Ziyambi alisema kuwa wafanyakazi ambao wanafikiria wana haki ya kuchagua ikiwa wanaweza kupewa chanjo au la wamekosea.

Serikali, ilianzisha kanuni mpya kwa makanisa na migahawa ili kuruhusu watu walio na kadi ya chanjo ndani ya majengo yao.

Lengo ni kukabiliana na changamoto ya watu kusita kuchanjwa.

Nchi hiyo ya Kusini mwa Afrika, imetoa chanjo kamili kwa watu milioni 1.7 pekee.

**BBC**

# WFP: Misaada chakula inahitajika Ethiopia

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

SHIRIKA la Chakula Duniani (WFP), limeonya kwamba mahitaji ya dharura ya chakula Kaskazini mwa Ethiopia, yanaendelea kuongezeka, wakati ghasia zikienea zaidi ya mipaka ya eneo la Tigray hadi kwenye majimbo jirani ya Afar na Amhara.

Shirika hilo linasema kwamba hadi watu milioni 7 wana uhaba mkubwa sana wa chakula huku wakikabiliwa na baa la njaa.

Watu hao ni pamoja na wengine zaidi ya milioni 5.2 walioko jimboni Tigray wanaotegemea msaada wa chakula kutoka Umoja wa mataifa ili kuishi.

WFP ilisema kwamba ghasia ambazo sasa zimeenea kwenye eneo lote Kaskazini mwa Ethiopia, zimesababisha watu wengine milioni 1.7 kukabiliwa na njaa.

Mwezi huu WFP imeanza kupeleka chakula cha dharura kwa watu Kaskazini mwa Ethiopia, ikiongeza kusema kwamba wanapanga kuwafikia watu 530,000 jimboni Afar pamoja na wengine 250,000 kwenye jimbo la Amhara.

Wakati huo huo, Msemaji wa WFP Tigary Tomson Phiri, alisema kwamba wakati hali ikiendelea kudorora, Mashirika ya misaada yanajitahidi kupeleka chakula cha dharura kwa zaidi ya watu milioni tano, kote kwenye jimbo hilo.

"Akiba ya chakula tulichokuwanacho kilikuwa karibu kumalizika siku mbili zilizopita hadi pale msafara wa kwanza wa msaada ulipofanikiwa kuingia jimboni humo baada ya muda wa wiki mbili. WFP iliongoza msafara wa zaidi ya malori 100 yakiwa na tani 3,500 za chakula pamoja na bidhaa nyingine kama vile dawa, mafuta na mahema," alisema Phiri.

Novemba 4, mwaka huu itakuwa mwaka mmoja tangu serikali kuu ya Ethiopia ilipoanza operesheni za kijeshi kwa nia ya kumaliza udhibiti wa TPLF kwenye eneo la Tigray.

**VOA**




Familia za wafungwa wapatao 41 waliokufa baada ya moto kutokea katika Gereza la Tangerang, nchini Indonesia lililoko pembezoni mwa mji mkuu wa Jakarta. Moto huo ulijeruhi watu 80 jana, huku wafungwa wengi wakiwa wamelala. **PICHA: XINHUA**

# Kesi washukiwa shambulio Septemba 11 yaanza tena

**Guantanamo,** CUBA

KHALID Sheikh Mohammad, kiongozi mwandamizi wa kundi la al-Qaida na anayedaiwa kuwa kiongozi wa mashambulio Septemba 11, anakabiliwa na kesi pamoja na washtakiwa wenzake mbele ya tume ya jeshi katika kambi ya jeshi la Marekani, Guantanamo Bay, Cuba.

Wanakabiliwa na mashtaka ambayo ni pamoja na kula njama, kushambulia raia, mauaji, utekaji nyara wa ndege na ugaidi. Ikiwa watahukumiwa, watapewa adhabu ya kifo.

Mchakato wa kusikilizwa kwa kesi hiyo kwa wale wanaotuhumiwa katika shambulio hilo, umekumbwa na tatizo la kisheria kati ya waendesha mashtaka na mawakili wa upande wa utetezi, kuhusu ni ushahidi gani unaweza kutumika.

Tofauti hizo zinahusisha masuala yote mawili ya nyenzo zilizoainishwa na utumiaji wa habari iliyopatikana wakati wa mahojiano, ambayo wanasheria wa utetezi wanasema ilipatikana kutokana na kuwatesa washukiwa

Mashambulio hayo yaliwahusisha wanaume 19 walio na uhusiano na Al-Qaeda wakiteka nyara ndege nne, na kugongesha mbili kati yazo kwenye majengo ya World Trade Center mjini New York, huku nyingine ikigonga makao makuu ya kijeshi Pentagon, nje kidogo ya Washington.

Ndege ya nne ilianguka katika uwanja jimbo la Pennsylvania. Mashambulio hayo yaliwauwa karibu watu 3,000.

Marekani ilijibu kwa kuanzisha uvamizi wa Afghanistan kulenga Al-Qaeda na kushinikiza Taliban, ambao walishutumiwa kuwapatia hifadhi magaidi, kuwasalimisha.

Operesheni za jeshi la Marekani nchini Afghanistan zilidumu kwa miaka 20 tu, zikimalizika mwishoni mwa Agosti mwaka huu, wakati Taliban wakichukua tena udhibiti wa nchi hiyo.

VOA

MECHI KALI
HOME
AWAY
MASH AL MUBAREK
2.31 | 3.09 | 2.95
FC ANDIJON

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 482



# ENRIQUE AMUITA GUARDIOLA KUINOA HISPANIA

**MADRID,** Hispania

LUIS Enrique ameeleza kwamba angependa kumwona Pep Guardiola akichukua mikoba ya kuinoa timu ya Taifa ya Hispania kwa siku za usoni.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona, Guardiola mwezi uliopita alibainisha kwamba, anatamani kufundisha timu ya taifa baada ya kuondoka pale Manchester City.

Mkataba wa sasa wa Guardiola na Man City unamalizika mwaka 2023, na wakati akipanga kuchukua likizo ya mapumziko akimaliza muda wake, pia anataka kupata uzoefu wa kufundisha timu ya taifa.

Enrique ambaye aliendeleza kile alichokiacha mchezaji mwenzake huyo wa zamani pale Camp Nou, amesema hana tatizo kumwachia mikoba ya ukocha wa timu ya taifa, Guardiola.

"Ningependa kumwona (Guardiola) akiwa kocha wa Timu ya Taifa ya Hispania. Napenda sana hilo litokee," alisema Enrique akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Kosovo.

"Nini zaidi, ninachopenda kuona ni timu yetu ya taifa kuwa na kiwango bora zaidi. Na naamini Hispania itakuwa na kocha bora zaidi kama yeye akichukua mikoba."

# LIVER KUVUNJA BENKI KWA BELLINGHAM



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL watatoa ada itakayoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 80 ili kumsajili kiungo wa kati, Bellingham kutoka Borussia Dortmund, limedai gazeti la Daily Star.

Nyota huyo wa klabu ya Borussia Dortmund ambaye ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya England, Bellingham amekuwa akicheza Ujerumani kwa zaidi ya miezi 12 sasa.

Hivi karibuni amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi England, baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Liverpool haikufanya usajili wa wachezaji wengi wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto, wakiwa wamemsajili mlinzi wa Ufaransa, Ibrahima Konate pekee.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mchezaji huyo wa England anawaniwa sana na kocha wa 'Wekundu' hao wa Anfield, Jurgen Klopp.

Na kama kitatolewa kiasi hicho cha fedha kwa usajili wa Bellingham mwenye umri wa miaka 18, ataweka rekodi ya kuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa fedha nyingi zaidi klabu hapo.

## HABARI MICHEZO

# ,274,020

# JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/21 | 17:00 | Brentford vs Brighton | 2.72 | 3.12 | 2.72 |
| 02. 11/09/21 | 17:00 | Watford vs Wolverhampton | 3.27 | 3.17 | 2.30 |
| 03. 11/09/21 | 17:00 | Southampton vs West Ham | 2.87 | 3.42 | 2.42 |
| 04. 11/09/21 | 17:15 | Ternana vs Pisa | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 05. 11/09/21 | 19:00 | Napoli vs Juventus | 2.56 | 3.46 | 2.66 |
| 06. 11/09/21 | 22:00 | Amorebieta vs Burgos | 2.42 | 2.95 | 3.10 |
| 07. 12/09/21 | 14:00 | Montpellier vs St Etienne | 2.44 | 3.38 | 2.79 |
| 08. 12/09/21 | 16:00 | Bordeaux vs Lens | 3.09 | 3.39 | 2.24 |
| 09. 12/09/21 | 16:00 | Brest vs Angers | 2.65 | 3.30 | 2.60 |
| 10. 12/09/21 | 16:00 | Spezia vs Udinese | 2.92 | 3.38 | 2.40 |
| 11. 12/09/21 | 17:15 | Osasuna vs Valencia | 2.51 | 3.07 | 3.02 |
| 12. 12/09/21 | 18:30 | VfL Bochum vs Hertha BSC | 2.93 | 3.23 | 2.41 |
| 13. 12/09/21 | 19:15 | Ponferradina vs Almeria | 2.80 | 3.30 | 2.41 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### ALHAMISI - 09 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:35 | 1152 | Zibo Sunday vs Nantong Zhiyun | 5.42 | 3.68 | 1.57 |
| 14:35 | 5739 | Sichuan Jiuniu vs Chengdu Qianbao | 5.02 | 3.67 | 1.60 |
| 14:45 | 3721 | Mash AL Mubarek vs FC Andijon | 2.31 | 3.09 | 2.95 |
| 15:30 | 1395 | Legion-Dynamo Makhachkala vs Anzhi Makhachkala | 2.81 | 3.15 | 2.37 |
| 17:00 | 1512 | Sportivo Iteno vs Deportivo Santani | 2.62 | 3.01 | 2.62 |
| 18:00 | 4411 | Maardu Starbunker vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.12 | 8.90 | 15.83 |
| 18:00 | 5588 | Limianos vs CDC Montalegre | 5.04 | 3.63 | 1.61 |
| 19:00 | 3029 | TuS Schwachhausen vs Werder Bremen III | 1.21 | 7.00 | 8.17 |
| 19:00 | 4687 | Justo Jose De Urquiza vs CA San Miguel | 2.23 | 2.70 | 3.62 |
| 19:30 | 4221 | Slavia Prague W vs Arsenal W | 9.69 | 7.17 | 1.17 |
| 22:00 | 3394 | La Equidad vs Deportes Tolima | 2.52 | 2.86 | 2.86 |
| 22:15 | 1946 | Afturelding Mosfellsbaer W vs FH Hafnarfjordur W | 2.42 | 4.16 | 2.26 |
| 22:15 | 5777 | HK Kopavogur vs Augnablik W | 2.25 | 4.50 | 2.55 |
| 23:00 | 4074 | Mineros Guyana vs Monagas SC | 2.81 | 3.49 | 2.21 |
| 23:00 | 4192 | AD Guanacasteca vs CS Herediano | 3.20 | 3.25 | 2.11 |

### IJUMAA - 10 - SEPTEMBA 2021

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1143 | Nagoya Grampus vs Tokushima Vortis | 1.78 | 3.20 | 4.56 |
| 19:00 | 3120 | Midtjylland vs Nordsjalland | 1.57 | 4.12 | 5.11 |
| 19:30 | 1725 | Oleksandria vs FC Ingulets | 1.88 | 3.68 | 3.44 |
| 20:00 | 1277 | Spartak Subotica vs Backa Topola | 2.54 | 3.27 | 2.54 |
| 20:30 | 4341 | Lokomotive Sofia vs Pirin Blagoevgrad | 2.00 | 3.39 | 3.34 |
| 21:00 | 1569 | Roda Kerkrade vs NAC Breda | 2.06 | 3.66 | 3.07 |
| 21:00 | 2548 | SBV Excelsior vs Dordrecht | 1.35 | 5.08 | 6.84 |
| 21:00 | 2631 | Emmen vs Maastricht | 1.42 | 4.71 | 5.89 |
| 21:00 | 2716 | Jong PSV vs Jong Ajax | 2.48 | 3.70 | 2.60 |
| 21:00 | 2890 | Telstar vs Almere City | 3.17 | 3.66 | 2.01 |
| 21:00 | 2928 | FC Oss vs ADO Den Haag | 2.26 | 3.32 | 2.93 |
| 21:00 | 2968 | VVV Venlo vs Den Bosch | 2.15 | 3.57 | 2.94 |
| 21:00 | 3196 | Jong AZ Alkmaar vs Jong Utrecht | 2.11 | 3.70 | 3.15 |
| 21:00 | 3252 | UTA Arad vs Rapid Bucuresti | 2.08 | 3.09 | 3.63 |
| 21:00 | 3715 | Brondby vs Silkeborg | 1.86 | 3.65 | 3.80 |
| 21:00 | 3988 | De Graafschap vs FC Volendam | 1.74 | 3.83 | 4.03 |
| 21:00 | 5062 | HNK Gorica vs Hrvatski Dragovoljac | 1.30 | 5.02 | 7.73 |
| 21:30 | 1092 | Benevento vs Lecce | 2.25 | 3.15 | 3.20 |
| 21:30 | 1175 | Bray Wanderers vs Athlone Town | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 21:30 | 2063 | Yverdon-Sport FC vs FC Aarau | 3.49 | 3.88 | 1.81 |
| 21:30 | 3772 | FC Stade LS Ouchy vs FC Schaffhausen | 2.25 | 3.42 | 2.80 |
| 21:45 | 1106 | Derry City vs Finn Harps | 1.94 | 3.24 | 3.68 |
| 21:45 | 1398 | Drogheda Utd vs Bohemians FC | 3.45 | 3.25 | 2.01 |
| 21:45 | 2470 | Caernarfon Town vs Cefn Druids | 1.14 | 7.38 | 12.62 |
| 21:45 | 2502 | UCD Dublin vs Cabinteely | 1.42 | 4.55 | 5.81 |
| 21:45 | 2670 | Cork City vs Shelbourne | 3.88 | 3.30 | 1.87 |
| 21:45 | 2777 | Glentoran Belfast vs Ballymena Utd | 1.43 | 4.70 | 6.60 |
| 21:45 | 2834 | Galway United vs Treaty United | 1.56 | 3.82 | 5.22 |
| 21:45 | 4430 | Brugge vs Oostende | 1.34 | 5.12 | 7.49 |
| 21:45 | 5683 | Sligo Rovers vs St Patricks | 2.85 | 2.95 | 2.47 |
| 22:00 | 1659 | Wexford Youths vs Cobh Ramblers | 3.19 | 3.38 | 2.06 |
| 22:00 | 1663 | Shamrock Rovers vs Waterford Utd | 1.30 | 4.75 | 8.72 |
| 22:00 | 3129 | Birmingham vs Derby | 1.86 | 3.20 | 4.43 |
| 22:00 | 5065 | Lorient vs Lille | 3.58 | 3.33 | 2.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# PIQUE: BARTOMEU ALIKUWA WA OVYO BARCA




**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique anaamini, Josep Maria Bartomeu ni miongoni mwa marais wa ovyo zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya Klabu ya Barcelona.

Bartomeu alichukua nafasi hiyo kuanzia Januari 2014 hadi alipojiuzulu Oktoba mwaka jana, huku pia akikumbana na kisanga cha kufikishwa mahakamani kwa madai ya rushwa.

Kujiuzulu kwake kulitokea baada ya tishio la Bodi ya Barca kutaka kupiga kura ya kutokuwa na imani naye.

Barca ilishinda mataji matatu katika mwaka wa kwanza wa Bartomeu katika kipindi chake cha miaka mitano hapo kwa miamba hao wa Catalunya.

Lionel Messi aliweka wazi uamuzi wake wa kutaka kuondoka kabla ya kukamilisha uhamisho wake wa kwenda Paris Saint-Germain, huku Pique akiwa ni mmoja wa wachezaji wachache walioamua kukubali kupunguziwa mishahara hapo Camp Nou kutokana na matatizo ya kifedha ya klabu hiyo.

Na sasa Pique amefunguka kwamba, Bartomeu alishindwa kufanya kazi yake kwa ufanisi klabuni hapo.

"Kwa kile kilichotokea wakati wake, unaweza kusema kwamba, ni rais wa ovyo zaidi," alisema Pique akiiambia La Sotana.

"Ni ukweli usiopingika na uzoefu nilionao, klabu imetipia wakati mgumu zaidi kwenye historia yake.

"Sasa nina matumaini na nina hamasa. Ndani ya miaka mitano ijayo au kumi mambo yatakuwa mazuri sana kwa Barcelona."




# PSG BADO YAKOMAA NA RICHARLISON

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain ya Ufaransa bado ina nia ya kumsajili mwaka ujao Richarlison de Andrade 'Richarlison' wa Everton.

Mawakala wa mchezaji huyo walifika Paris wiki iliyopita kwa ajili ya mazungumzo ya uwezekano wa uhamisho huo wa majira ya joto yajayo.

Richarlison anapigiwa debe kuwa mbadala wa Kylian Mbappe anayehusishwa kuondoka PSG mara mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Mbappe ameshaonyesha wazi nia yake ya kutaka kuondoka hapo Paris na kituo chake kinachofuata ni kule Madrid.

Na hivyo, PSG wanaona kwamba Richarlison nyota wa timu ya Taifa ya Brazil, ndiye mchezaji pekee anayeweza kuziba pengo la Mbappe.

Mbappe amebaki PSG na Richarlison bado yupo Everton kwa sasa huku hatima ya wote wawili ikitarajiwa kubadilika mwaka 2022.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDES ACHAMBUA RONALDO KURUDI UNITED

●●● Tunajua ari itakuwa juu, tunajua nini anachoweza kutupa sisi, kila mmoja anajua Cristiano ana...

**MANCHESTER, ENGLAND**

KURUDI kwa Cristiano Ronaldo pale Old Trafford kutaongeza ujasiri na kusaidia Manchester United kushinda mataji, kwa mujibu wa Bruno Fernandes.

Fernandes alikuwa mchezaji nguzo wa United msimu uliopita, akifunga mabao 18 na kutoa pasi za mwisho 12 kwenye Ligi Kuu England wakati kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kikimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo.

Ronaldo sasa ameungana na mchezaji mwenzake huyo wa timu ya Taifa ya Ureno, aliyerudi hapo Manchester baada ya miaka 12, awali akifunga mabao 118 kwenye mechi 292 kwenye mashindano yote katika kipindi chake cha kwanza kucheza hapo.

Na Fernandes, ambaye alionyesha kiwango cha juu na kutengeneza pasi tano muhimu na asisti moja wakati Ronaldo akikosekana kwenye mchezo wa timu ya Taifa ya Ureno dhidi ya Azerbaijan, amesifia ubora na ujasiri wa mfungaji huyo wa wakati wote wa timu ya taifa.

"Tunajua kwamba, ari itakuwa juu, kila mmoja anajua Cristiano ana furaha kubwa na kujiamini sana bada ya kurudi tena hapa," alisema Fernandes akiiambia RTP3.

"(Sisi) wachezaji ni sehemu ya ujasiri huo, tunajua nini anachoweza kutupa sisi. Malengo yetu ni makubwa na Cristiano pia, kwa sababu nilichoongea naye ni kuhusu kushinda mataji.

"Malengo yetu yatabaki kuwa hivyo, kwa uwapo wa Cristiano, kuna kitu cha ziada cha kutusaidia kufika kule tunakotaka kwenda."

Ronaldo mwenye miaka 36, anaweza kucheza mchezo wake wa kwanza Septemba 11, mwaka huu dhidi ya Newcastle United, klabu ambayo ndio pekee kwenye Ligi Kuu England aliyoifunga mabao matatu 'hat-trick' kabla ya kuondoka Manchester mwaka 2009.

## ZISIKUPITE

### DAKA AOTA MBAWA LIVER

HATUA ya Liverpool kushindwa kumuuza winga wa Uswizi, Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 29, au mshambuliaji wa Ubelgiji Divock Origi, 26, imewafanya wakose nafasi ya kumsajili mshambuliaji Patson Daka wa Zambia mwenye miaka 22 kutoka Red Bull Salzburg, kabla ya kujiunga na Leicester City. **(Here We Go Podcast, via Express)**

### ADEYEMI AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Liverpool ni miongoni mwa klabu tatu ikiwamo Bayern Munich na Barcelona zinazopania kumsajili nyota kinda wa Red Bull Salzburg na Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 19, ambaye amefunga mabao sita katika mechi sita za Ligi Kuu msimu huu. **(Bild, via Mirror)**

### KOUNDE LAZIMA CHELSEA

CHELSEA wataendelea kumfuatilia mchezaji wa Sevilla, Jules Kounde mwenye umri wa miaka 22, kwa lengo la kumnunua Januari baada ya kumkosa mlinzi huyo msimu huu wa majira ya joto. **(Evening Standard)**

### SABABU CITY KUMKOSA SILVA

KLABU ya Manchester City imemkosa, Wesley Ribeiro Silva msimu huu baada ya dau lao la pauni milioni 6.5 la kumnunua winga huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 22 kukataliwa na Palmeiras. **(Marca, via HITC)**

### BELLINGHAM HUYOOO LIVERPOOL

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18, amedokeza kuwa huenda akajiunga na Liverpool huku kocha, Jurgen Klopp akijiandaa kuvamia klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund. **(Star)**

### ELNENY MAMBO MAGUMU

ARSENAL wamekataa dau lililowasilishwa na klabu ya Uturuki ya Galatasaray kumnunua kiungo wa kati wa Misri, Mohamed Elneny mwenye umri wa miaka 29. **(Sky Sports)**

### ASENSIO AIKATAA SPURS

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25, amekataa nafasi ya kujiunga na Tottenham Hotspur au AC Milan msimu huu wa majira ya joto. **(Marca)**

### UNITED WAPEWA RICE

MANCHESTER United wamepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, msimu ujao baada ya Chelsea kuelekeza darubini yao kwa mchezaji mwingine. **(Mirror)**

### MAVROPANOS KUJIFUNGA STUTTGART

MLINZI wa Arsenal aliyesahaulika, Mgiriki Konstantinos Mavropanos mwenye umri wa miaka 23, huenda akapewa mkataba wa kudumu katika klabu ya Stuttgart ambayo sasa anaichezea kwa mkopo. **(Bild, via Star)**

### ONUACHU ANUKIA ANFILED

LIVERPOOL pia wamepewa nafasi ya kumsajili mshambuliaji mwenye umri wa miaka 27 wa Genk na Nigeria, Paul Onuachu. **(Mirror)**

HABARI MICHEZO

## Klabu tisa kushiriki mtifuano kuogelea

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya klabu tisa zitashiriki katika mashindano ya wazi ya Klabu Bingwa ya Taifa yaliyopangwa kufanyika katika Bwawa la Kuogelea la Klabu ya Gymkhana Septemba 25 na 26, mwaka huu.

Klabu hizo ni Dar es Salaam Swim, Taliss, Champions Rise, Mwanza Swim na Arusha Swim, pia kuna klabu za Mis Piranhas, Bluefins na, FK Blue Marlins, kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Chama Cha Kuogelea Tanzania (TSA), Khadija Shebe.

Shebe alisema mashindano hayo yatashirikisha waogeleaji wenye umri kuanzia miaka tisa na wenye miaka 15 na zaidi katika mashindano hayo yamedhaminiwa na Samsa Logistics Limited, Sapphire Court Hotel limited, Selcom Paytech Ltd, Pepsi, Azam, Gymkhana Club, Tarmal Industries Ltd, Tanpack na Flames Restaurant.

Alisema kutakuwa na makundi manne, kundi la miaka tisa na 10, 11 mpaka 12, 13-14, na 15, ambapo muogeleaji atakayeibuka wa kwanza atapata pointi 20, wa pili na tatu watapata pointi 16 na 14 kila mmoja.

## Benki NBC yarejesha tabasamu kwa watoto

**Na Jumanne Juma**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imejipambanua tena kuwa ni taasisi inayojali jamii kwa kurejesha kiasi kidogo cha faida kwa dhumuni la kufadhili programu na miradi mbalimbali nchini, hiyo ikiwa ni kutokana na sera zake.

Hayo yamebainika jijini Arusha katika mbio za Nyika zilizoratibiwa na kuandaliwa na Taasisi ya Same Qualities iliyojikita katika kutoa huduma za upasuaji bure kwa watoto wenye tatizo la mdomo wazi maarufu kama mdomo sungura

Akizungumza baada ya kukamilisha mbio za kilomita 10, zilizoanzia na kuishia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid huku zikihudhuriwa na wadau mbalimbali kikiwamo Chama cha Riadha Mkoa wa Arusha, Meneja wa Tawi la NBC Meru, Florence Ng'wavi, alisema wametoa kiasi cha Sh. milioni 22.5 zitakazopelekwa kugharamia upasuaji wa watoto takribani 30, ili kuwarejeshea tabasamu zao kwenye huduma za upasuaji zitakazofanyika katika kambi maalum za matibabu zilizoratibiwa na Taasisi ya Same Qualities, Mikoa ya Tabora, Moshi na Shinyanga kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Alisema: "Lengo letu katika kutoa msaada huu kwanza ni kurejesha tabasamu kwa watoto hawa pamoja na familia zao, pia ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kufikisha huduma mbalimbali kwa jamii za Kitanzania".

# POULSEN ATAKA STARS KUGEUZA KWA MKAPA KUWA 'MACHINJIO'

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' Kim Poulsen, amesema anataka kuugeuza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuwa sehemu ya 'machinjio' (wageni kupoteza) katika michuano iliyopo mbele yao.

Stars juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Madagascar, mchezo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa wa kutafuta tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2022, zitakazofanyika nchini Qatar.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi baada ya ushindi huo, Poulsen alisema anaamini kila mechi ni muhimu kupata matokeo mazuri na malengo yake ni kuona anatumia vema uwanja wa nyumbani kuwa sehemu ya machinjioni kwa timu ngeni zitakazokuja kucheza, dhidi ya Stars.


"Niwapongeze sana wachezaji kwa kufuata maelekezo yangu baada ya kwenda mapumziko tukiwa 2-2, wakati tulipokuwa tunaongoza, walirudi nyuma jambo ambalo halitakiwi katika soka, niliwaeleza tunaenda kipindi cha pili kuhakikisha tunashambulia na kushambulia, jambo ambalo tumefanikiwa kupata ushimdi.

"Jambo lingine nimewasisitizia kwa sasa tunataka kutumia Uwanja wa Benjamini Mkapa kuwa sehemu ya machinjio kwa yeyote anayekuja, hatoki na ushindi," alisema Poulsen.

Alisema ameona mabadiliko makubwa kwa wachezaji wake kuongeza kujiamini na kufuata maelekezo anayowapa, hivyo kuwataka kutumia vema uwanja wa nyumbani kupata matokeo mazuri katika mechi watakazocheza kwa Mkapa.

"Kwa kujiamini kwa wachezaji wangu, natarajia mechi zijazo kucheza vizuri na kutafuta matokeo, kwa sababu wapinzani tunakutana nao (Benin) ni wagumu," alisema kocha huyo.

Matokeo hayo yanaifanya Stars kukaa kileleni mwa Kundi J ikiwa na pointi nne sawa na Benin, ambayo wanalingana hadi tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalum Benki ya NMB, (Head of Private Banking), Getrude Mallya, akimkabidhi mfano wa hundi ya thamani ya Sh. milioni 25.5, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, ikiwa ni udhamini wa Mashindano ya Mchezo wa Gofu ya Mkuu wa Majeshi 'NMB CDF Trophy 2021'. Kulia ni Meneja wa Club ya Gofu ya Lugalo, Luteni Kanali, Frank Kaluwa na Meneja Mwandamizi Wateja Maalum wa NMB, Emmanuel Mahodanga, wakishuhudia. Benki ya NMB imetoa takribani jumla ya Sh. milioni 60, kwa ajili ya udhamini wa mashindano hayo kwa mwaka huu. **MPIGAPICHA WETU**

# NMB yanogesha mashindano ya Gofu Lugalo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa Sh. milioni 60, kwa ajili ya kudhamini mashindano maalumu ya Mchezo wa Gofu ya Mkuu wa Majeshi 'NMB CDF Trophy 2021', yanayotarajiwa kuanza Septemba 17 hadi 19, mwaka huu kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu vya Lugalo jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

Mashindano hayo ambayo hufanyika kila mwaka, lengo kuu ni kuuinua mchezo huo pamoja na kukuza vipaji vya wachezaji chipukizi, ili kuja kuwa tegemeo kwa taifa kwa siku zijazo.

Akizungumza kwenye hafla ya kukabidhi hundi ya udhamini huo, Mkuu wa Kitengo cha Wateja Maalumu wa NMB, Getrude Mallya, alisema wanajisikia furaha kuwa sehemu ya kufanikisha kufanyika kwa mashindano hayo, ambayo anaamini mwaka huu yatafana kutokana na zawadi nono, ambazo zimeandaliwa kwa washindi.

Mallya alisema kiasi hicho cha fedha kimetumika katika kununua vifaa mbalimbali vitakavyotumiwa na washiriki wa shindano hilo ikiwamo fulana, kofia, bendera na zawadi za washindi, ambazo zitatolewa siku ya mwisho.

"Sisi kama NMB tunajisikia furaha kuona shindano la mwaka huu linakwenda kufanyika kwa ubora na mafanikio ya juu kabisa na hii inathibitisha kwamba sisi ndio Benki, ambayo inaijali jamii kwa ukaribu kutokana na kudhamini masuala mbalimbali ikiwamo ya kimichezo," alisema Mallya.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Michael Luwango, alisema zaidi ya wachezaji 170, wanatarajia kushiriki mashindano ya mwaka huu ikiwamo vijana wadogo wa shule (Junior), ambao wao ndio watakaofungua mashindano hayo siku ya kwanza Septemba 17, mwaka huu.

"Siku ya ufunguzi itakuwa kwa vijana wadogo Junior) unajua wameanza mitihani sasa wakitoka huko vichwa vimechemka, wanaweza kuyatumia mashindano haya kujipooza na siku itakayofuatа, ambayo ni Septemba 18 na 19 ndio itakuwa zamu ya wakubwa na wale wachezaji wakimataifa endapo watajisikia ilimradi kufuata taratibu zinazotakiwa ikiwamo kulipa ada," alisema Luwango huku akieleza mkapa sasa walіomba na kuthibitisha kushiriki wamefikia 100 kutoka klabu 10 tofauti nchini.

Naye Katibu wa Chama cha Gofu Tanzania (TGU), Boniface Nyiti, alisema shindano hilo la Mkuu wa Majeshi lipo kwenye Kalenda ya TGU na limekuwa na mchango mkubwa kwa taifa kutokana na kutoa wacheaji wengi, ambao wanajenga timu ya taifa.

# Michezo

Alhamisi Septemba 9, 2021

Nipashe




Fernandes amchambua Ronaldo United

UKURASA 22

LUIS VS BANDA...



Kiungo wa zamani wa Simba, Luis Miquissone, akimiliki mpira dhidi ya nyota wa sasa wa klabu hiyo, Peter Banda, wakati timu yake ya Msumbiji ikichezea kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Malawi kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar iliyopigwa Uwanja Orlando, Soweto nchini Afrika Kusini juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Gomes apagawa na ubora nyota Simba

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI nyota wake wa kimataifa wakitarajiwa kuanza kuwasili leo baada ya majukumu ya timu zao za taifa, Kocha wa Simba, Didier Gomes, amesema anafurahishwa na juhudi za nyota wake tangu kuanza kwa kambini msimu huu.

Baada ya kurejea kutoka Morocco, Simba kwa sasa imeweka kambi mkoani Arusha kujiandaa na msimu mpya wa ligi na michuano ya kimataifa.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi baada ya mazoezi ya jana asubuhi, Gomes alisema wachezaji wake wameonyesha uchu mkubwa wa kufanya vizuri kwenye ligi kutokana na namna wanavyojituma na kufanyia kazi maelekezo yake.

"Tangu tukiwa Morocco wachezaji wangu wamekuwa wakinionyesha uchu wao, wamekuwa wakipambana mazoezini na kila mmoja anaonyesha uchu wa kufanya vizuri.

"Sina tatizo [la ubora] kwa mchezaji yeyote, kila mmoja anajituma kwa kweli hili ni jambo jema kwangu mimi kama kocha na kwa benchi la ufundi kwa ujumla," alisema Gomes.

Aidha, alisema ameomba kwa uongozi kucheza angalau michezo miwili ya kirafiki ikiwezekana na kutoka nje ya nchi ili kupima kikosi chake.

"Najua kuna mchezo wa Simba day, lakini nikipata na mwingine mapema itakuwa vizuri naamini viongozi wanafanyia kazi," alisema.

# YANGA: PIGO KUMKOSA AUCHO, DJUMA, MAYELE

## ●●● Uongozi wawahi Fifa huku mashabiki nao wakiwekwa kiporo kuingia uwanjani Jumapili hadi...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema ni pigo kubwa kwao kuwakosa wachezaji watatu, Khalid Aucho, Shabani Djuma na Fiston Mayele kwenye mechi za Kombe la Shirikisho Afrika wakianza dhidi ya Rivers United ya Nigeria, lakini tayari wamewasilisha barua Shirikisho la Soka Duniani (Fifa), kuomba kushughulikiwa haraka kwa Hati za Uhamisho wa Kimataifa, (ITC) za nyota hao.

Wachezaji hao hawataruhusiwa kucheza mechi ya Jumapili wiki hii kutokana na barua za kuruhusiwa kusajiliwa na Yanga kutoka kwa klabu zao za awali kuchelewa kuwasili, hivyo kuichelewesha Yanga kuwasilisha maombi ya ITC zao kutoka Fifa.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, alisema bado hawajakata tamaa kuhusu kupata ITC ya nyota hao baada ya kupeleka barua Fifa kuomba suala hilo kushughulikiwa mapema.

"Kutokana na sababu ambazo ziko nje ya viongozi wa Yanga, tumechelewa kupata ITC za nyota hao kutoka Fifa na kuziwasilisha CAF. Hivyo tumeomba Fifa kutusaidia katika hilo ili ndani ya siku hizi kuzipata.

"Kuwakosa nyota hao ni pigo kubwa, lakini hatuwazi sana kwa sababu tayari Kocha Nasreddine (Nabi) kawaandaa nyota wengine kuziba nafasi zao," alisema Manara.

Alisema msimu huu wamejipanga vizuri na kulingana na usajili mkubwa walioufanya kwa kusajili wachezaji zaidi ya watatu katika nafasi moja, hawana presha endapo watawakosa nyota hao.

"Kuzuiwa kwa Aucho ni kutokana na Klabu ya Misr Lel Makkasa ya Misri kuchelewesha [barua ya kumalizana naye] kama ilivyokuwa kwa AS Vita [na Djuma]. Yanga iliomba kwa wakati uhamisho huo, lakini Waarabu hao awali waligoma kumwachia Aucho na kuibuka mgogoro mkubwa kwa pande hizo mbili, huku kesi ikiwa kubwa hati ikatolewa tayari muda wa dirisha la usajili ukiwa umeshafungwa," alisema Manara.

Alisema kosa kama la Aucho lilifanyika tena nchini DR Congo kwa klabu za AS Maniema Union na AS Vita nazo hazikutuma kwa kuthibitisha kwa wakati ruksa ya kufanyika kwa uhamisho wa Djuma na Mayele.

Kuhusu viingilio vya mchezo huo wa Jumapili, Manara alisema wamechelewa kuweka wazi viingilio vya mechi hiyo kwani wanasubiri taarifa kupitia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kutoka CAF, juu ya idadi ya mashabiki watakaoingia uwanjani.

"Tunatambua ni mechi muhimu kwetu, hivyo tumejipanga vizuri lakini tumeshindwa kutaja viingilio kwa sababu hadi tupate taarifa TFF, kwa sababu ya changamoto ya COVID-19," alisema Manara.

Alisema kulingana na umuhimu wa mchezo huo wanakuja na kauli mbiu ya 'The Return of Champions' (Mabingwa Wanarejea), kuhakikisha wanafikia malengo yao matatu kwa msimu huu.

"Malengo hayo ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na kuvuka hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hili suala la kukosa ubingwa mara nne mfululizo msimu huu hatukubali na tumejipanga vizuri," alisema Manara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042